# MBEGU YA DHAMBI



# MBEGU YA DHAMBI

# TAWASIFU

Mwandishi wa kitabu hiki, Henry Murigi Kariuki alizaliwa mwaka wa 1960 katika kitongoji kidogo cha Marumi, kaunti ya Murang‟a. Alisomea shule ya msingi Marumi iliyo karibu na nyumbani.
Alifanya mtihani wa CPE (Certificate of Primary Education) na baadaye akajiunga na shule ya upili ya Githima. Hakuweza kuyatimiza masomo ya shule ya upili kwa sababu ya kukosa karo.

Katika harakati za kuishi, alihuzunishwa na mwongozo wa ulimwengu. Baada ya kusikia na kuangalia katika mitandao vile ambavyo watu wanaangamizwa na kuangamizana wenyewe kwa kutojua kiini cha mpagao huo.

Hapo, akaona ulimwengu umezama kwenye bahari. Basi, hapo ndipo alipatwa na mawazo ya kukusanya nakala zenye suluhu au zenye kueneza ujumbe katika ulimwengu.

Alifanya juhudi kubwa, usiku na mchana, kuandika hayo mawazo katika hiki kitabu. Kwa hivyo, angependa kumshukuru Mola kwa kumpa moyo mkunjufu ili habari hii iwafikie wengi.

# DIBAJI

**SURA YA 1: MBEGU YA DHAMBI** ---------------------------------------------5

**SURA YA 2: MAUMBILE** ------------------------------------------------------- 7

**SURA YA 3: MBEBA NAJISI** -------------------------------------------------- 9

**SURA YA 4: WANANDOA KUTENGANA**-------------------------------------- 12

**SURA YA 5: MADHEHEBU POTOVU**----------------------------------------16

**SURA YA 6: DESTURI** ---------------------------------------------------------19

**SURA YA 7: JINSI WAELEKEZI WANATENGANISHA** ------------------23

**SURA YA 8: UTAMADUNI WA KUOA**----------------------------------------25

**SURA YA 9: FUMBO LA MAISHA** --------------------------------------------26

**SURA YA 10: UPOTOVU WA ULIMWENGU** ---------------------------------33

**SURA YA 11: VITA VYA NIGERIA** --------------------------------------------- 38

**SURA YA 12: VITA VYA SOMALIA**-------------------------------------------40

**SURA YA 13 :VURUGU BAADA YA UCHAGUZI NCHINI KENYA** ----42

**SURA YA 14 : SAFARI YA KISIASA YA UHURU KENYATTA** ---------- 44

**SURA YA 15 : UBORA WA MAISHA KWA ULIMWENGU** ---------------57

# SURA YA 1: MBEGU YA DHAMBI

Sisi wote, tumewahi kuusikia au kuufahamu mmea unaoitwa dhawani na kujua tabia zake. Tabia zake huenea haraka na kujizungushia kwenye mimea ingine, kuimalizia maji na mbolea hadi kukauka. Huu mmea, unaweza kujitafutia maji na mbolea, kwa vile hupitia chini ya mimea ingine. Wakati mkulima ameona tabia ya mmea huu, yeye hushtuka mara moja kwa kujua kuwa, hatakuwa na mazao shambani mwake. Kuepukana na shida hii, inampasa kuung‟oa na kuuchoma. Naye Mungu, hafurahishwi na uwepo wa dhambi ulimwenguni, ambayo huondoa neema aliyompatia mwanadamu. Hii ni laana ambayo huelekeza watu kukosa kujua na kuziheshimu familia na wazazi wao. Huwa wanaheshimu wakubwa wa mashirika na madhehebu wanayoyaegemea.

Dunia imezingirwa na taabu kwa sababu wenye kuelekeza, ndio pia huipotosha jamii. ***Badala ya kuhimiza upendo wa mtoto kwa mzazi, (mwenye mizizi ya upendo) wao huelekeza upendo kwa wapita njia ama pasipostahili, baadaye huyo mtoto huachwa bila upendo kwa mzazi.*** Mara nyingi wenye kuaminika, badala ya kuonyesha miujiza ya Mungu, huonyesha miujiza ya ubinadamu, ambayo hujaa sarakasi za kupendeza macho.

Haya makosa, ndiyo yaliyomfanya Mungu kukasirika na kuadhibu nchi za Sodoma na Gomora. Kwa kukosa heshima na maadili mema, walianza kujamiana wanaume kwa wanaume na wanawake kwa wanawake. ***Ulimwengu umewapotosha wanadamu mpaka, hawaelewi upendo na baraka zilizo na mizizi.*** Vilevile, hawajui laana ni nini kwa maisha yao, kama vile wanasodoma na Gomora walivyokosa kutofautisha kati ya mke na mume kwa raha zao za ngono.

Watu hawa hufanya vijana kuachwa bila mwelekezi na kubaki kulaumiwa na kudharauliwa. Baadaye, hao vijana hujiunga na vikundi sugu kama vile, Alkaida, Jihad, Alshabaab, Mungiki na vinginevyo.

Vikundi hivi, wakati mwingine hupata ufadhili kutoka kwa wapinduzi au wapinzani wa serikali iliyo mamlakani. Vile vile, kuna vikundi vya wauzaji mihadarati, ambao huungana ili kupata nguvu. Kumaanisha nchi zenye utawala mbaya hua zinachangia kuongezeka kwa ujambazi (ulaghai) kwa vijana.

Hii ina maana kuwa, nchi yenyewe baadaye haiwezi kuwazuia na badala yake huwapa nafasi ya kufanya biashara haramu, bila wasiwasi. Kwa hivyo, nchi zinafaa kuungana, ili kuwazuia magaidi kupata nguvu zaidi. Jambo hili, lilidhihirika wakati taifa la Marekani lilipokuwa likiwinda magaidi wa kundi haramu la Alshabab. Marekani ilitumia raslimali nyingi. Nchi ya Somalia ilihangaishwa na kikundi hicho cha Alshabab hadi, ikamulazimu Rais Siad Barre kusalimu amri na kuiacha nchi hiyo ikiwa imezoroteka kiuchumi. Baada ya Alshabab kutawala kwa muda, walianza kushika

mateka meli za nchi zingine baharini. Hapo ndipo, umoja wa mataifa (UN) uliingilia zoezi hilo na kikosi cha AMISON mwaka wa 2007. ***Tukio hili linadhihirisha vile ambavyo ulimwengu umejaa laana ambayo imeleta vifo na uhabilifu mkubwa kwa jamii.***

Bado, hii shida imetokana na ulimwengu kupuuza uhusiano wa kifamilia, kama wafanyavyo wanyama; kutofahamu mama ama baba. Hapa ndipo watu wanafaa kuelewa ama kujua umuhimu wa kuuheshimu ubinadamu wao. Ni vizuri watu waelewe ya kwamba, vile ambavyo binadamu anazeeka, ndivyo ambavyo dhamiri ya roho hupata nguvu ya kutenda kwa kusema ama kuwaza juu ya mwenye kumfanyia vibaya.

***Baadaye mwenye kuwaziwa huingiwa na mapepo ya mwenye kumuwaza. Hili, humfanya mwenye kuwaziwa, kuwa mpagawa kwani, mawazo ya kupiga taswira huwa yamepotea. Wakati mwingine, watu hawafahamu kuwa mwili hauna nguvu za kujiendeleza, bali huendeshwa na dhamiri ya roho ambayo hupotoshwa na mapepo, yanayobadili mienendo ya mtu. Hivyo basi, mtu huyo anaweza kupotoka, kwani, maumbile yake huhusisha watu wawili, ambao ni Mungu muumba na mwanadamu mwenzake(mzazi), katika kuleta kiumbe kingine duniani. Hao wako na uwezo wa kubariki na kulaani, kwa njia ya kusema ama ya kukimya kulingana na tabia ya mwenye kuwaziwa mienedo yake.***

## Kupotoka

Jambo la kupotoka hutisha jamii sana kama mmoja wao ameadhirika na upotovu. Kwani, wao hujua yeye sio mtu wa kutegemewa tena. Hii ni kwa sababu, ni vigumu kufahamu chanzo cha shida kama hii. Na watalaamu wa magonjwa hufanya juhudi za kutafiti chanzo cha hizo shida, na hata wakati mwingine huwatuma wagonjwa nyumbani kwa kukosa suluhu. Hivyo basi, magonjwa haya yakizidi, inabidi wazee wajulishwe ili wapeane historia ya mwadhiriwa. Hii hufanyika ndio isiwe ni jambo la kinyumbani.

# SURA YA 2: MAUMBILE



*Maumbile ya Binadamu*

Katika maisha ya mwanadamu, kuna dhamiri tano ambazo husaidiana, ili awe mkamilifu kimaisha. Dhamiri hizi, hukua kulingana na vile mwili hupata malezi bora yanayoambatana na mahitaji ya mwili. Dhamiri hizi ni kama vile;

***Dhamiri ya kuona*** - Dhamiri ya kuona huambatana na ya kufikiria na ya roho, ili kukata kauli. Dhamiri hii, ni kama kamera za cctv, macho yakiwa ni kama dirisha ama kio cha kupitia mwangaza. Dhibitisho ni, kufungua macho, kama haiambatani na dhamiri ya roho. Mwenye kufungua hawezi kutafakari ameona nini.

***Dhamiri ya kusikia*** - Dhamiri ya kusikia na ya kufikiria huafikiana na ya roho, ili kukata kauli. Dhamiri hii yaweza kufananishwa na kinasa sauti, kile ambacho, husikia sauti na kuihifadhi ili baadaye kutafsiriwa.

***Dhamiri ya kuhisi*** - Dhamiri ya kuhisi hushirikiana na ya roho, ili kukata kauli. Dhamiri hii yaweza kufananishwa na kioo cha mguzo (touch screen) ile huonyesha msisimko baada ya kuguzwa. Msisimko wakati mwingine huletwa na fikira, kama kuna jambo la kushtusha kama vile kifo. ***Mtu kama anatumia dawa za kulevya, msisimko huongezeka, ambapo baadaye, msisimko huo hupotea na hufanya akili kukwama. Bangi ama dawa za kulevya ni nyepesi, kwa kuchanganyika na damu, sio kama sigara.*** Sigara huwa na moshi ile hubaki kwa mapavu, lakini dawa za kulevya ama bangi, huingia kwenye damu na kuharibu ubongo.

***Dhamiri ya kufikiria*** - Dhamiri ya kufikiria hushirikiana na ya roho, ili kukata kauli. Dhamiri hii huwa ni kama tarakilishi (computer), ile huhitaji usaidizi wa zile zingine, ndio iweze kupokea, kugawa na kutafakari mageni.

***<u>Dhamiri ya Roho</u>*** - Dhamiri ya roho husaidia hizo zingine kwa uamuzi wa kutenda. Dhamiri hii, yaweza kukua kuliko zile zingine. Kwa sababu hiyo, wenye dhamiri hizi, hujulikana kama watu wa maono. Kundi hilo huwa na wahubiri wakubwa, wachawi na pia wale wanaojulikana kuwa wajuaji. Dhamiri hio yaweza kufananishwa na damu ile huhitajika mahali popote kwa mwili. Pia, hupea zile zingine nguvu, kwa kutenda na kutafakari, na ndio huamua mtu ni wa aina gani kwa kuzaliwa. Dhamili hii ndio hupokea mageni na kuweka kwa ubongo, kama ubongo ni mwepesi kwa kupokea.

Ukiona mtu haelewi ama ni mjinga tangu kuzaliwa kwake, inamaanisha kuwa ni dhamiri fulani haikukomaa. Mara nyingi, dhamiri hii huwa ya roho, na ndio inayoshikilia zile zingine. Dhamiri hukua kwa pamoja, na watu wengi huwa kwa kiwango ambacho dhamiri zote ziko sawa. Watu huwa kawaida kuweza kupata utaratibu wa maneno. Dhamiri zote hukufa, isipokuwa ya roho. ***Dhamiri hiyo, hubeba madai na maagano, baada ya mwenye dhamiri kufariki. Dhamiri hiyo huwa, inawaongoza watu walioachwa.***

Kwa sababu ya hayo, unaweza kuwaona watu wengine wakifanya maajabu ama miujiza, na kati ya hao kuna wale ambao hufanya miujiza ya Mungu, ilhali wengine huwa na nguvu za waliokufa. Kuna wengine ambao, hujishughulisha na mahitaji ya mapepo na kuwahifadhi kama biashara yao. Hata hivyo, kuna roho ambayo, huongoza miungano ya wanakiapo, hasa wakati ambapo, wengine kati yao wameaga dunia. Roho hiyo hukinga wenye kutii na kuheshimu makubaliano yao. Hali kadhalika, mtu anaweza kulaaniwa kwa kutotii.

***Mwanadamu huonekana kuwa mkamilifu kwa sababu ya kuzaliwa na mtu. Lakini, binadamu ni roho ambaye, ni dhamiri iliyojificha ndani yake, ndio awe mwongozo katika hali yoyote ya maisha. Kwa hivyo, kama kuna mambo kwa familia au nasaha, ni hiyo dhamiri huwa inatawala kulingana na mwenye kuacha madai. Hii dhamiri, huleta ujumbe wa mwenye kubarikiwa na mwenye kulaaniwa katika jamii yoyote.***

Hatari ya maisha huanza wakati mmoja amekosea dhamiri (kukaidi waliokufa) kwani, huanzisha familia na laana. Hapa ndipo hutokea familia ya wezi, wachawi, na mambo mengine mabaya katika jamii.

# SURA YA 3: MBEBA NAJISI



*wauaji*

Mbeba najisi, ni mtu ambaye amelaaniwa na mtu ama watu kulingana na makosa aliyoyafanya au yaliyofanywa hapo awali na wazazi wake yaliyohuzunisha ukoo. Kwani kwa kila ukoo kulikuwa na mambo kadhaa yaliyokuwa mwiko kuyatenda na, hali kadhalika kuyasema. Waliokiuka sheria hizo lazima wangepatwa na laana. Kuna watu mbali mbali waliojipata katika shida hii pamoja na familia zao, baada ya kupuuza kutoa mahari kwa wakwe kama ilivyo desturi. Wengine ni wale waliohusika kuwaua ndugu zao ili waridhi mali yao. Vile vile kina mama wengine wale waliowaua mabwana zao ili wapate uridhi. Mara nyingi, watu wa aina hii hupatwa na laana ambayo huadhiri familia zao au wao wenyewe.

***Basi, baada ya mtu kulaaniwa, uzao wake hutoka ukiwa umepatwa na mpagao, ama kujipata katika nafsi ya kuleta ujumbe wa mambo yale wazazi waliyoyafanya. Ujumbe huu waweza kutolewa kwa matendo au kwa kusemwa bila wasiwasi wowote, kwa maana mwenye kuutoa ujumbe huwa katika nafsi nyingine ya kutojielewa. Kwa sababu ya hali ya kutojielewa, yule mtendaji au msemaji huwa hazingatii heshima wala kuwa na uwoga.***

Kwa mfano, mtu aliyelaaniwa anaweza kumpiga, kumuua au hata kumtukana mzazi wake lakini, iwe hafanyi kwa kupenda ama kutarajia. Shida kubwa, hutokana na matendo yaliyotendwa na wazazi wake na hawakufikiria kuomba msamaha, ili akatize uchungu walioupitia wazazi kwa ajili yake.

Watu wa aina hii ni hatari sana. Kwani, mtu mwenye kutaka kuoa ama kuolewa anaweza patana nao bila kujua wala kutarajia. Hii ni kwa sababu, watu hawa hawana tofauti na watu wengine isipokuwa kukosa dhamiri ya kuyatambua makosa. Hatari nyingine ya watu hawa ni kuwa wanaweza kuchochewa na magenge ya vijana ambao huonekana kukosa uwoga, na pia huwa hawarudi nyuma katika kutimiza jambo walilolipanga.



*mwenye majuto*

Mara nyingi vijana hutumbukizwa katika majuto na wanasiasa bila kujua mwenye kuwafanyia hivyo ako na nia yakujipendekeza. Kwa hivyo yeye huwapa nguvu ya kufanya jambo lolote wanalolitaka. Wanasiasa hupendelea vijana ili kuwatumia kuwaondoa wapizani wao. Katika harakati hizo, wao huwatumia vijana kutekeleza jambo. Mambo huzidi kuchacha wakati wameshirikiana na watumishi wa umma wafisadi. Kwani vijana huwapatia nguvu zaidi za kuharibu raslimali na kuhangasha raia.

Wakati mwingine, vijana hudanganyika na kushawishika na vikundi vya watu, kwani mara nyingi wao huwa na pesa za kughalamia raha za kila aina. Ni kawaida pia,

kuwapata hawa vijana wakichochea vurugu na kupeleka dawa za kulevya shuleni pamoja na kuanzisha migomo, kuchoma madarasa na mabweni kwa vile hawana haja na yale masomo.

Cha kushangaza ni kuwa, ni vigumu kutofautisha kati ya yule asiye na laana na mwenye laana. Yote haya hujitokeza wazi na kugunduliwa baada ya migogoro ya mambo mabaya kufanyika. Ulimwengu umebeba mambo mengi mazito kwani, katika harakati ya kuishi lazima mtu aishi na kila aina ya watu. Sio rahisi kuweza kufahamu mienendo na mawazo yao, ila tu kuishi nao.

Shida kubwa, ni kuoa ama kuolewa na mtu mwenye laana ilhali hakuna muda au nafasi ya kuchunguzana kikamilifu. Jambo hili hujitokeza mara nyingi iwapo wanandoa wamekuwa pamoja au pengine wamepata watoto. Hapo ndipo, changamoto huanza kujitokeza polepole.

***Kama ni laana, mengi huwa ni malipo ya maovu yaliyofanyika hapo awali. Kama mmoja alimpiga au kumtukana mzazi, hilo latarajiwa kumafanyikia mwanawe. Kwa hivyo, atakuwa ametumbukia katika laana pamoja na mpenzi wake. Mambo haya huchanganya maisha ya wanaopendana ama wanaotaka kuishi pamoja, kwa kuwa wengi huwa hawafahamu chanzo cha kusumbuana au kutengana.***

# SURA YA 4: WANANDOA KUTENGANA



*utengano kati ya wanandoa*

Kuna mambo ambayo huwapata wanandoa bila kutarajia kwa kutojua ama kutoelezewa. Hili jambo la kutengana hupata familia nyingi, kwa sababu zifuatazo;

**Laana**

**Ngono**

**Magonjwa**

**Viungo**

**zaidi Ukali**

**Wazazi**

**Uvivu**

## Laana katika ndoa

Laana huleta tatizo kubwa katika familia au jamii, na hili ni jambo lisilojulikana na watu wengine. Familia yaweza kuwa na vita au utengano, lakini chanzo cha mambo hayo yote haijulikani, labda iwe, kuna wazazi au wazee walioacha madai, mwongozo, mwelekeo ama msemo na hawapo tena. Kwa mfano, waweza kuwa katika ndoa kwa muda, kisha ukawasahau, ukuwatenga wazazi au kupuuza kutoa mahari. Kwa sababu hiyo, mapepo yanaweza kutoka kwa ukoo na kuvuruga amani katika jamii. Shida Kama hii, yaweza

kujitokeza, iwapo hawa wanandoa walifaa kutimiza jambo fulani. ***Hali kadhalika, kuna familia ama ukoo usiooa au kuolewa kwa sababu ya mambo yaliyofanyika hapo awali.*** Jambo hili hukosa kueleweka kwa walio katika ndoa, kwani huwa hawagundui mambo mpaka yanapoenda mrama. Wanaweza kuyafahamu hayo iwapo tu, wataielewa historia na kanuni za familia. Familia inaweza vurugwa na mtu mwenye wivu na akasababisha janga. Hii bado, ni hali isiyoeleweka kwa kuwa mwenye kutenda haya huwa anajificha na kuyafanya kisiri.

## Ngono katika ndoa

Kulingana na maumbile, kila kiumbe hakina uwezo wa kuzaa kivyake, kwani lazima kuwe na jinsia kinzani. Mtu huzaliwa na mwenzake ambaye kupitia ngono. Kwa hivyo ngono hua na manufaa yafuatayo;

- ***Kuunganisha***: Hili jambo haliwezi kuelezeka, kwa sababu, huingia kwa mawazo ya binadamu na kumfanya kumuwaza mwenzake. Ngono humfanya mwanamke na mwanaume kuelewana bila masharti yoyote, hata wanapokasirishana au kukosana. Vile vile, ngono hufanya wenye kuwiana au kuoana wawe na uaminifu na furaha kwa vile watapata kizazi. Maumbile ya mwanadamu huwa ni jambo fiche na Mungu, kwani vile mwanamme na mwanamke huungana na kuishi pamoja kila mmjoa akiacha watu wao. Hili ni jambo la ajabu. Jambo hili ndilo likipatana na ngono huwa na nguvu. Zaidi ya hayo, mambo haya hufanya watu kufunguliana roho na kuwa hawana siri tena kwa kila mmoja. Ngono hutumika kama parafujo ama bisibisi ile hupenyeshwa kwenye mwanya ndogo na baadaye kuwa mwanya kubwa. Ngono pia huunganisha ndio kupata uzao na ulezi pamoja katika maisha ya mwanadamu, na pia kwa wanyama.
- ***Kuzaa***: Ili watu wazaane ni lazima kuwe na ngono kati ya wawili. Mwanaume na mwanamke hutoa mbegu ili kuendeleza kizazi. Mambo haya hutendeka kwa viumbe vyote vyenye uhai na lazima pawe na kiumbe cha kiume na cha kike. Kwa hivyo, mmoja wao akiwa na kasoro ya kimwili kama vile kuwa tasa ama gumba, huwa hiyo familia haiendelei kwa sababu hakuna anayeridhisha mwenzake. Hapo ndipo mwenye kasoro huwa anakataa kuungana na mwingine, katika ndoa kwa sababu ya aibu.
- ***Kutuliza***: Baada ya mme na mke kuwaziana, fikira huleta hisia kwa mwili. Jambo ambalo huwafanya washiriki ngono, ili kuwatuliza. Hii ni dhibitisho kuwa ngono ina manufaa katika ndoa.

Katika maumbile ya kila kiumbe, Mungu amekiumbia kiumbe kizani na kuwekwa roho ya kufanya kila kimoja kitafute na kiwaze kingine kama tulizo. ***Hamu ya ngono huwa, kama kamba ama nyororo ya kuvuta ama kushikanisha ndio kukalisha pamoja. Hapo***

***ndipo mwanadamu huzidi, kwani hutumia akili ya kutafakari umuhimu wa maisha.*** Katika maisha ya mwanadamu, mtu humchukua mwenzake kama raslimali, kwa maisha na utulivu wa akili.

## Magonjwa katika ndoa

Kulingana na maumbile ya mwanadamu, kuna magonjwa ambayo huwa ya kawaida ambayo huadhiri wanadamu kwa wingi. Hali kadhalika kuna magonjwa hatari kama vile kifafa, uwazimu na ukimwi ambayo hufanya watu kupeana taraka.

## Viungo zaidi katika ndoa

Kwa bahati mbaya, watu wengine huzaliwa wakiwa na viungo vya uzazi zaidi ya kimoja, cha kike na cha kiume. Mara nyingi huwa ni vigumu kugundua, lakini kama mmoja amegunduliwa huachwa na wenzake hata kama sio kupenda kwake. Kwa hivyo, hili jambo husababisha kuvunjika kwa ndoa, kukosa kuoa au kuolewa.

## Ukali zaidi katika ndoa

Ukali kupita kiasi hufanya familia kushindwa na kujiendeleza wala kupanga jambo mwafaka kwa kukosa kuelewana. Shida kubwa ni kuwa mwenye ukali hajijui jinsi alivyo. Hali hii ikiwa kwa mwanamke, hiyo familia haiwezi kuendelea na huishia kwa kugombana na vita vya kila siku. Iwapo mmoja wao hatanyenyekea, hiyo familia haitasimama.

Ukali hutokana na damu na mawazo ya mtu, na huwa wakati mwingine ni hatari, kama mmoja ni mjinga wa kuzaliwa, kwani hashauriki wala kuambiwa. Ukali waweza pia kutokana na ugonjwa wa akili, ambao hufanya watu kushindwa kujua kinachoendelea kwa muadhiriwa.

## Wazazi katika ndoa

Swala la wazazi ni lingine ambalo hufanya wapendwa kutengana. Jambo hili huwapata wazazi kwa sababu, wao hufwata maswala ya familia za watoto wao. Wakati mwingine, msichana aliyeolewa katika familia anaweza kukosa heshima kwa mavyaa ama bavyaa. Mume anaweza kuwa, hana uwezo wa kujimudu kimaisha ila kutegemea wazazi. Jambo hili hufanya mzazi kushughulika na majukumu ya wanao. Hatimaye, kusababisha kuvunjika kwa ndoa. Vile vile kuna baadhi ya wazazi waliopuuza kutoa mahari kwa ukoo. Hali hii husababisha kuvunjika kwa ndoa ya uzao wao.

## Uvivu katika ndoa

Wanandoa hutarajia familia yao iwe yenye usafi, kuvutia na ufanisi. Changamoto hutokea wakati mmoja wao akiwa mvivu. Uvivu ni jambo ambalo husababisha kuvunjika kwa ndoa, kwa njia nyingi. Mme au mke kutowajibika katika majukumu yao, kama vile kuzembea kikazi au kukwepa kazi. Uvivu hutokana na ubongo kuwa mzito kwa kutenda ama kufikiria. ***Na ndio, ujinga ni uzito wa ubongo kushindwa kutafakari. Mtu mwenye uzito wa ubongo huwa hana mambo mingi hata ya kuongea, na hupenda kulala.*** Kwa hivyo, usifurahie kuwa na mtoto mwenye kulala ovyo ovyo, kwa sababu anaweza kuwa na shida ya uzito wa ubongo ama ugonjwa. Ubongo ndio huendesha mtu afanye ama atende jambo, hualifu mwili. Kwa hivyo, mmjoa akiwa mvivu, kuelewana na mwenzake hua ni shida.

Kuna uvivu mwingine wa kimwili na huenda ukaisha kulingana na vile mtu amefanya mazoezi mengi. Uvivu huu ndio mara nyingi huwa na watu matapeli, malaya, wakora na wahubiri wauongo. Baadhi yao ni kama Jim Jones, Paul Makenzi, Bonnie Nettles, Credonia Mwerinde, Joseph Kibwetere na wengine ambao watazidi kuchipuka, kama viongozi waulimwengu hawana shughuli na wanadamu wakiangamizwa, na hawa wenye madhehebu potovu.

# SURA YA 5: MADHEHEBU POTOVU



Jim Jones

James Warren Jones, aliishi kutoka mwaka wa 1931 hadi 1978, alikuwa kiongozi wa dhehebu potofu lililojulikana kama, the Peoples Temple (Hekalu la watu), kutoka mwaka wa 1955 hadi 1978. Aliwaongoza wafuasi wake kwa kile kilichojulikana kama "*revolutionary suicide*" ambapo aliwamrisha kunywa dawa ya sumu, ambapo, watu zaidi ya 900 walikufa. Jim Jones, akishirikiana na wafuasi wake wakaribu, kuweka mikakati ya mauwaji kwa washirika wa dini yake, iliyokuwa katika mji wa Guyana, eneo la Jonestown mnamo mwaka wa 1978. Matendo ya Jim Jones yanaufahamisha ulimwengu mzima, matokeo ya makundi na madhehebu potovu.

"The Good News International" ya Paul Makenzi katika eneo la Shakahola Kilifi mkoa wa pwani.



*Paul Mackenzie*

Makenzi aliongoza dhehebu la kidini lililotoa mafunzo potofu kwa wafuasi wake. Waumini wa kanisa hilo walidai kuwa walilazimika kufunga kama sehemu ya kufuata mafundisho jambo ambalo, lilisababisha maafa ya watu zaidi ya mia nne (400), kutokana na ukosefu wa chakula na maji. Ingawaje, hakukuwa ushahidi wa moja kwa moja ya kusimamia madai haya, video kadhaa za Mchungaji Makenzie zilipatikana, ambapo, makenzi aliamuru watu wafunge. Lakini, kuna ujumbe unaorejelewa mara kwa mara kuwasihi wafuasi kutolea sadaka kile wanachothamini, ikiwa ni pamoja na maisha yao.

Mada nyingine ya mahubiri tata ya Mchungaji Mackenzie, ilikuwa ni wazo kwamba elimu ni ya kishetani na hutumiwa kupora pesa. Mnamo 2017 na 2018, alikamatwa kwa kuwamrisha watoto wasiende shule kwani alidai, "***elimu haitambuliki katika Biblia***". Mchungaji Mackenzie pia amelaani elimu kwa kuendeleza mapenzi ya jinsia moja kupitia programu za elimu ya ngono. Harakati za serikari kuingilia kati, zilisababisha kukamatwa kwa Makenzi pamoja na wafuasi wake na kufunguliwa mashitaka kotini. Mashtaka hii ilipata nguvu baada ya kupatikana kwa vifo vya watu vilivyosababishwa na kunyimwa hewa na kugongwa na vifaa butu kichwani.

## Heaven's Gate

Dhehebu la kidini la Heaven's Gate (Lango la Mbinguni) katika eneo la Southern California, pia ni kundi lililotambulika kuendelesha masomo potofu ya kidini. Mnamo mwaka wa 1997, washiriki 39 wa dhehebu la Heaven's Gate katika eneo la San Diego, California, walijiua kwa wingi kwa kutumia sumu, wakizingatia hii, kama ishara ya kuondoka kwao kutoka Duniani. Waliokufa ni pamoja na mwanzilishi mwenza wa dhehebu hilo, aliyejulikana kama Marshall Applewhite. Bonnie Nettles, ambaye alikuwa ni mwanzilishi mwingine wa madhehebu ambayo yalioamini kwamba, washiriki wangeweza kujigeuza kuwa viumbe vya nje visivyoweza kufa, kwa kukataa asili yao, ya kibinadamu, alikufa kutokana na ugonjwa wa saratani mnamo mwaka wa1985.

## Mauaji ya kidini ya Kanungu nchini Uganda yaliyoua wafuasi 700





*Credonia Mwerinde* *Joseph Kibwetere*

Mauaji mabaya ya kidini duniani, yalifanyika kusini magharibi mwa Uganda katika wilaya ya Kanungu mnamo mwaka wa 2000, ambapo baadhi ya wanachama 700 kutoka Vuguvugu la Kurejesha Amri Kumi za Mungu (The Movement for the Restoration of the Ten Commandments of God), walichomwa moto hadi kufa. Washiriki waliamini kwamba, ulimwengu ungefikia mwisho mwishoni mwa milenia ya 2000, walifungiwa ndani ya kanisa, na milango na madirisha yakafungwa kwa nje. Kisha badaye, jengo hilo likawashwa moto. Waumini hao walivutiwa na viongozi wenye hisani Credonia Mwerinde, mhudumu wa baa na mfanyakazi wa ngono wa zamani, na mfanyakazi wa zamani wa serikali Joseph Kibwetere, ambao, walisema walikuwa na maono ya Bikira Maria, katika miaka ya 1980. Waliandikisha Harakati kama kundi ambalo, lengo lake lilikuwa kutii Amri Kumi na kuhubiri neno la Yesu Kristo.

Madhehebu haya, yamechukua mwanya kwa watu, juu ya umaskini na wengine uvivu, ilhali wanataka utajiri kwa njia ya miujiza. Hali hii ya umaskini imefanya raia watumiwe vibaya, hata wengine kutolewa kafara na watumishi wa aina hii. Wahubiri hawa hutumia wafuasi wao kama, watoto wale ambao hudanganywa na wazazi wao ya kwamba, wanaweza kupiga mtu yeyote achezao nawao na hali wakijua ule ni msemo tu, hana uwezo wowote wa kumlipishia mtoto.

Madhehebu haya, huchukua mwanya baada ya kung‟oa washirika kutoka kwa ukoo wao, baada ya ukoo kuzingiziwa kuwa na uchawi, ujinga na mambo yanayomsaliti Mola.

# SURA YA 6: DESTURI



*baraza la wazee*

Desturi ama utamaduni hutumika kama mwongozo katika maisha ya mwanadamu. ***Baadhi ya desturi huwa ni maagano ya wazee wa jamii kote ulimwenguni. Desturi ama utamaduni huwekwa na wazee waliomakinika katika ukoo na hujadiliwa wazi katika baraza lao la wazee, kwa manufaa ya jamii zao.*** Baada ya wazee hawa kufariki, desturi hii, huwa kama sheria, na yapaswa kuzingatiwa na walio hai.

Majadiliano haya hufanya desturi kuwa ni maono ya kuhakikisha jamii yao iko na amani. Viongozi wa familia walipaswa kudumisha utamaduni huu kwa sababu desturi huwa ni maono mazuri ya wazee wa ukoo. Wazee hawa walihakikisha familia zao zinafuata mafunzo hayo ili kuwaepusha na laana. Walioshiriki katika kuunda desturi hizi walikuwa na busara nyingi na waliwatahadharisha watu kuwa, atakayekosa kufuata desturi hizo angepatwa na janga ama shida ya aina fulani.

Wazee wa ukoo walipendekeza heshima kwa wazazi kutoka kwa watoto wao na kwa mtu yeyote katika jamii. ***Katika miungano ya wazee, mambo yaliyozingatiwa sana ni laana, ulinzi na mambo mengine ya kuhifadhi jamii kwa amani na umoja.***

Katika mikutano yao, wazee walizingatia ubora wa maisha ya watoto, ili wasipatwe na laana na malumbano ya familia. Kuna jamii ambazo, zilikuwa zikikiuka sheria za ukoo na baadaye kupatwa na laana. Shida zaidi ni kuwa, watoto wao mara nyingi walizaliwa wakiwa na mapepo yaliyowafanya watukutu. Kwa hivyo, hawa watoto walikuwa wakizileteа familia zao laana na vurugu.

Ni jambo la ajabu kwa kuwa, katika jamii ya sasa, watoto wa aina hii wapo katika shule za msingi na vile vile vyuo vikuu, bila ya walimu kuwatambua kuwa, wana tatizo hili. Watoto hawa huonyesha umaarufu wa hali ya juu, kuchochea watoto wengine kuzitamani tabia zao bila kutambua mambo hayo kwa undani. Wanafunzi wa tabia hizi huchangia pakubwa, kwenye migomo mashuleni na vile vile kuleta vurugu bila kuogopa kwani, hawana haja na masomo na pia maisha yao.

Shida hii huumiza wanafunzi wanaotilia maanani shuleni na wale ambao wazazi wao ni maskini. Wale ambao wazazi wao ni matajiri huweza kupata nafasi katika shule zingine kwa urahisi, kwa sababu wana uwezo wa kifedha. Hali hii imeukumba ulimwengu mzima hata kama kuna wataalamu wa aina nyingi, kama vile wanasaikolojia, lakini hawawezi kutatua shida hii, kwani hukua pole pole na mwenye shida huwa hana habari.

***Hapo awali, mzazi aliposhuku kuwa mtoto amekumbwa na shida hii alipaswa kufanya uchunguzi, ili afahamu kiini cha mambo yale na kutambua ikiwa laana imetoka katika jamii ama makosa ni ya mtoto. Wakati mwingine angefuata kiini cha jina la mtoto, ili apate suluhisho kutoka kwa ukoo.*** Lakini, kama mtu angekubaliana na desturi ya wazee hangekwazika. Kwani ni Wazee wa ukoo waliokua wakifunza heshima na utaratibu wa kuishi kwa yeyote bila kubagua umri, ili mtu asipatwe na laana. Katika miungano ya wazee, jambo walilokua wakizungumzia, lilikuwa kuepusha watu wote na laana ama kukosana katika jamii.

***Ukoo ulimtambua mjomba kama mzazi wa pili kwa mtoto. Jambo hili, liliwapa wajomba uwezo wa kuwabariki watoto***. Mjomba alikuwa na manufaa sana, kwani angesaidia kuwalea watoto hao na kuboresha maisha yao bila tatizo lolote. Yeye angesaidia kupeana watoto kwa ukoo, ili wapate baraka na vile vile kuwashauri iwapo, walikuwa wameanza kuwa na utukutu. Iwapo kuna kitu chochote kilihitajika ili wabarikiwe, basi mtoto au mama yake angemwomba mjomba kupeana. Kwa hivyo, mjomba alikuwa na manufaa mengi hivi kwamba, mtoto angewalemea wazazi, yeye angetekeleza jukumu hilo kulingana na utaratibu wa ukoo.

***Ukoo ulitambua kuwa, mtoto mwenye utovu wa nidhamu na heshima angeleta laana na baadaye matatizo ya kila aina kwa ukoo.*** Ilikuwa ni makosa sana, mtu kukosea, kwa sababu, ukoo ulifahamu kuwa, anajikosea yeye mwenyewe na pia familia yake na ukoo kwa jumla. Mtu huyu angepata laana ambayo ingehangaisha jamii. Ukoo uliamini kuwa, mtu mbaya alichangia kuleta familia mbaya, ukoo mbaya na hatimaye ulimwengu mbaya.



*Mjomba akimshauri mjukuu wake*

Kwa mfano, aliyekuwa rais wa Uganda Idi Amin Dada ambaye aliushtua ulimwengu kwa mauaji mengi, kwa kupiganisha wanadamu bila huruma wala uwoga wowote. Watu kama hawa waliaminika na ukoo na pia ulimwengu mzima kuwa hatari sana. ***Iliaminika kuwa uzuri wa mtu, huanzia katika ukoo wake, na mtu hawezi kuwa mzuri ulimwenguni iwapo, yeye angekuwa ni mbaya katika familia na ukoo wake.*** Kwa mfano, mtawa MotherTeresa alionyesha wema wake kote ulimwenguni, na alikuwa ameuanza katika kijiji chao, ambapo alikuwa amezaliwa kama wasichana wengine walioolewa na kupata mabwana na utajiri wa dunia.



*Mtawa Mother Teresa*

Yeye alijinyima na akajitolea kuwa mtumishi wa mungu. Huyu mwanamke, alituliza roho za watu wengi maskini, bila kuwabagua kwa misingi ya kidini wala kabila. Ingawa kazi hiyo ingali inaendelezwa na watawa wengine. Swala hili la kujitolea na kujukumika, kwa njia yeyote ya utumishi lazima litokane na mtu kuwa na utu (*ubinadamu*). Ili kuwa na ukamilifu huu lazima uwe;

**Umezaliwa na binadamu**: Kiumbe chochote kinapozaliwa huwa, kinapata nafsi na hisia kutoka kwa kiumbe kilichokizaa na pia kuiga tabia za kiumbe hicho, mienendo na viungo vyake kwa jumla huambatana na vile vya mzazi. Hisia hizi ndizo hufanya kutambulika kwa aina ya mtu ama aina ya mnyama. Vile vile, hisia huvutana na ndio, kama ni mnyama hufuata na kupenda mnyama wa aina yake. ***Kwa binaadamu, hisia zake hulaani ama hubariki. Kwa mfano, ukitendea wema wazee, kipofu ama kiziwi, neema hukufuata***.

**Umelelewa na binadamu**: Malezi ni muhimu sana kwa mtoto kwani, nafsi na hisia zake pia hukua kulingana na ulezi wa walezi wake. Nafsi na hisia hizi humsaidia mtoto kupokea mawazo mageni katika maisha yake. Ni vizuri pia kwa walezi wa watoto kuwapa vyakula vizuri na vya kuboresha afya yao, ili kuipa miili yao nguvu za kutosha. Kiumbe chochote ukitaka kufunga, ama kushika akili yake, ni lazima ukilishe vyema. Hisia ya kula ndio yenye nguvu nyingi kwa mwili, kwani hata zile zingine hushikamana na ya kula ili kufanikisha malengo. Hii inamaanisha ya kwamba, huduma ya kwanza ya kila kiumbe ni kukilisha vyema, ili uweze kubadilisha akili ama mawazo yake ***itaambatana na namna ya mwenendo ama pahali na mazoea ya kuishi. Kwa mfano, kama mtoto wa mwanadamu anaweza kulewa na mnyama, kama vile nugu, akili yake yaweza kubadilika na kuwa kama ya mnyama huyo.***

**Umeshauriwa na binadamu**: Ushauri kwa mtoto huchangia pakubwa katika kukuza nafsi na hisia zake. Basi, akipata ushauri maalum, nafsi na hisia zake humwezesha kukabiliana na tatiso lolote katika maisha yake, kama vile anachokisikia, anachokiona na kukisema. Katika kuchanganua ushauri, mtoto huonyesha tabia zilizo sawa na zile za mzazi wake. Ni jambo la manufaa sana kwa, mzazi kumwonya mtoto na kumuadhibu kwa kiboko iwapo amekiuka ushauri. Mtu anapokua, anapaswa kuungana na wenzake, ili waweze kupata mawazo mema. La sivyo, anaweza kupatana na watu wengine wenye mawazo mabaya yatakayochangia matendo maovu. ***Shida iliyopo ni, kuwa mtoto amebakia mikononi mwa walimu, wahubiri na serikali huku mzazi akionekana kutengwa na kupewa majukumu chanya tu kama kumpa mtoto malazi, chakula na kumlipia karo.*** Jambo hili, husababisha mtoto kuwakosea wazazi heshima kwa sababu pengine, hawakusoma na labda wao hufanya kazi za vibarua. Basi, mtoto kama huyu huonyesha heshima zaidi kwa walimu na wahubiri. Iwapo atajitenga na hao, basi atabaki na mzazi yule asiyemheshimu, ingawaje chochote anachohitaji kutoka kwa mzazi, serikali itamulazimisha mzazi hata kama mwenyewe hakutaka kumpa. Basi, kitu hicho, kitakuwa kimetoka kwa mzazi bila baraka. Hatimaye, mzazi anaposumbuana na mtoto kwa muda, yeye humrushia mikono, kumaanisha amemlaani. Shinda kubwa, hawa huwa wametemwa na wazazi, wengine ndio wenye mashirika yenye uchungu na ukoo. Hawa wakishirikana na wale wamesoma huwa wanajaribu kubomoa ukoo, kama hawajahudumiwa na wao, ama sio wazazi.

# SURA YA 7: JINSI WAELEKEZI WANATENGANISHA



*Mwanasiasa akiwaongelesha wananchi*

Viongozi wa dini, wanasiasa na wanasayansi, hushauri wafuasi wao kupuuza na kuepukana na mafunzo ya ukoo. ***Viongozi hawa hawazingatii wala kuchanganua yale mafunzo mazuri yanayotokana na ukoo hata ingawa wafuasi wao wanayategemea au kurithiwa mali inayohifadhiwa na ukoo.***

Kuwa mcha Mungu ama kusoma sana halifai kuwa jambo la kusababisha mtu kujitenga na ukoo ama familia yake inayofuata mafunzo ya ukoo. Kupata hayo, yafaa kumfanya mtu kuwa mfano kwa wengine. Mtu kama huyo, anafaa kusisitizia wengine yale mazuri yatokanayo na ukoo na kuyakemea yale mabaya kwa heshima, kwani katika maumbile ya binadamu, uhai na amani ndio msingi wa maisha ya binadamu. Kwa hivyo, kuwa umesoma ama kua mchamungu, ndio unafaa kuwa msingi wa ushauri katika mambo mbalimbali kama: -

i. Heshima kwa maisha ya binadamu

ii. Haki baina yao kwa misingi ya upendo

iii. Maendeleo na utaratibu wa maisha

Muumbaji alitaka, jamii iwe na heshima na mawazo mazuri katika maisha, ili mwanzo wao wa ubinadamu uwe baba na mama ili waweze kuwashauri na kuwalea hadi kukomaa. Mungu alimpa kila mmoja majukumu yake, na uwezo wa kulea watoto vyema.

***Hili lamaanisha kuwa, ni vigumu mtoto kupata ukamilifu wa maisha, hasa kuwa na heshima kama hatalewa na wazazi wote wawili, ingawa katika jamii ya sasa, jambo hili halizingatiwi kwa makini na walezi wengi. Mtoto kama huyo, mara nyingi hukua na matatizo kama;***

**Ukali:** Ukali huwa na manufaa sana unapotekelezwa kwa njia inayofaa lakini, wengi huutumia vibaya na hivyo, ni lazima mtoto aelekezwe jinsi ya kuutumia, kwa kuonywa, unapopita kiasi. Ukali ukizidi, huwa unaonyesha madharau, kwa sababu haubagui kati ya mkubwa na mdogo. Hili jambo la ukali, huwekwa nguvu baada ya mhusika kufahamu kuwa, anayebishana na ye ni wa kiwango cha chini kimaisha. Mambo haya huzidi, kwani huyu mmoja akiwa mwoga, huwa na uwoga zaidi.

**Ujeuri:** Ujeuri hupoteza watoto, kwani huwa wanafuata mawazo na fikira zao, kwa kudhani kuwa zina manufaa. Hivyo basi, ni vyema wazazi kuwapa onyo kali na ushauri.

**Upotovu:** Utovu wa nidhamu hasa kwa watoto, huwa ni jambo hatari sana kwa mtoto na jamii yake. Mtoto kama huyo hupata laana kutoka kwa watu mbalimbali anaojihushisha nao. Watoto huhitaji kupewa onyo kali na ushauri na ikizidi waadhibiwe ili kurekebisha tabia, la sivyo watapotoka.

***Mtoto anapodumisha nidhamu na heshima kwa jamii, yeye hupata mawazo mazuri kuhusu maisha ya baadaye.*** Lakini, mtoto mpotovu ama anayejihushisha na matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vya uhalifu mara nyingi huwa ni shida kwa jamii ambayo husababishwa na **laana yake, laana kutoka kwa jamii, na kujihushisha na ulimwengu.**

Mtoto anapokua, huwa anapata baraka ama laana kutoka kwa watu wa aina mbalimbali. Hapo awali, wazee walifuatilia mienendo ya watoto kwa kina. Mara nyingi, mtoto anaweza kuadhiriwa na makosa ya mzazi ambaye hakutii mienendo ya ukoo na akapatwa na laana. Mtu kama huyu huiletea familia mikosi ya aina nyingi.

Jamii yaweza kuwa haina shida, lakini mtoto aungane na watoto watukutu. Hili hufanya mtoto apatwe na laana. Hivyo ndivyo familia zilikua zikichunguza mienendo ya familia zingine, ili waepushe watoto wao na familia potovu. ***Katika ukoo, mtoto alikuwa akilindwa na watu wote kama kiungo muhimu katika jamii na ukoo.*** Akikomaa, alikuwa akifunzwa utamaduni wa ndoa, ili aanzishe familia iliyo na baraka kutoka kwa watu.

# SURA YA 8: UTAMADUNI WA KUOA

Katika jamii ya sasa, baadhi ya watu hupuuza utamaduni wa ndoa. Wengi wao huitazama ndoa kama biashara ambapo kuuza na kununua huwa ndicho kitu cha maana kwao. Wengi hutafuta ushauri kwa watu wasiofaa, kama vile kijana anaweza kutafuta ushauri kutoka kwa watu wasiojua, badala ya kuenda kwa ukoo. ***Kuoa ama kuolewa ni jambo la kitamaduni, kwa kuwa dhabihu hutolewa, ili kubadilisha mahari na baraka.*** Hili hufanya uzao wa mwenye kuoa uendelee na uenee kwa ukamilifu wa aina zote za maisha. Ili baraka iwepo, lazima pawe na maelewano kati ya ukoo wa mme na wa mke.

Maelewano yalikuwa yakifanyika kwa namna ya kupeleka mahari kati ya wenye kutoa na wenye kuyapokea. Swala hili lilikuwa lifanyike ili dhabihu iwe kulingana na utaratibu wa mila. Ukoo ulikuwa ukifuatilia mambo haya ndio pasiweko na mikosi katika harakati hizo. Bado, Ukoo ulikuwa unafuatilia familia yenye kupokea mahari kama imewahi kupokezana kwa wale imetoa mwenye kuolewa ili pasiweko na dosari. Utaratibu huu ulikuwa unafuata ndugu na dada, kama wazazi wao hawako, kwa kupokea mahari. Mtu kama huyu, alikuwa anafuatiliwa asijaribu kuzuilia ndugu ama dada yake asipokee mahali bila kujua ukweli na utaratibu wa mila.

***Dhabihu bado, ilikuwa inatumika kushikanisha ukoo wa mke na mme. Ilikuwa ni lazima wakule na wakunywe pamoja kama sherehe.*** Katika sherehe hiyo, kuna vitu vya mashemeji vya kula au kunywa. Baada ya hayo, bibi na bwana hupelekwa mbele ya umati na kushangiliwa na watu wote pamoja. Hapo ndipo, wazee wa ukoo zote waliwaelekezea baraka kwa njia ya tabiko na kuwatemea mate ama kuwamwagia damu ya kondoo aliyechinjwa, juu ya dhabihu, kulingana na ukoo ama kabila. Kisha wao wangeachiliwa wakaanzishe familia kama wamepata ushauri kutoka kwa wazee. ***Hii humaanisha ya kwamba ukoo umepanda mbegu ambayo imezingirwa na mbolea (baraka) ili itoke ikiwa na kizazi cha kutegemewa na jamii ama ulimwengu kwa jumla.*** Mtoto alipozaliwa, akina mama wa rika moja na mama wa mtoto huyo, walikuwa wanamwamkua kwa vigeregere na shangwe, na kumpeana kwa wazee wa ukoo ndio afanyiwe tabiko la kumuondolea mikosi kulingana na utamaduni wa ukoo huo.

Familia nyingi zimekuwa na matatizo ya kila aina bila kukumbuka au kuwaza juu ya jambo hili la mababu. Kizazi cha sasa kimetupilia mbali tamaduni zao kwa sababu wamesoma na ilihali wanataka kuridhi mababu zao, wakisahau msemo ya kwamba "*baniani mbaya, kiatu chake dawa*."

# SURA YA 9: <u>FUMBO LA MAISHA</u>

Ulimwenguni kuna mambo mengi ambayo huwasumbua wanadamu bali, huwa hawaelewi sababu. Mambo hayo ni kama;

- Umalaya
- Vifo
- Magonjwa
- Ubakaji
- Ndoto
- Matokeo ya baraka au laana
- Sababu ya ulevi

**Umalaya**



*ukahaba*

Kuna kundi fulani la watu ambalo hufahamika kama malaya au kahaba ingawa watu wengi hawajui, kuna mambo ya aina tofauti huchangia mtu kuwa hivyo. Mambo hayo ni kama;

## <u>Kutojiheshimu</u>

Ulimwenguni, wanawake wasiojiheshimu ama kujijua wanazidi kuongezeka. Sababu ya kuwa namna hii, wengi wao ni laana huwaletea pepo ya kutojijua mpaka wanashindwa kujua uchi ni nini. Wao huishi maisha yasio na heshima, bora ajue kuishi kwa raha na starehe atakavyo. Mara nyingi, shida humpata mwenye kutaka kuoa, kwani huyu mwanamke hupatikana haraka, kwa sababu ya uzoefu wake wakutimiza haja za kimwili,

ilihali hana haja na kuolewa. Watu wa aina hii wanaweza kupotezea wenzao wakati wao na raslimali.

**<u>Shida za familia</u>**

Kuna wengine wenye heshima, ila kwa sababu za kijamii hufanya au kufanyiwa jambo ambalo halifai. Kwa mfano, wakati mwingine anaweza kupatana na mtu asiyefahamu mahitaji ya familia, na zaidi ya hayo, anataka kula na watoto wake wapate elimu.

Hii shida yaweza kumzidi mpaka aanze kujiuza, ili mahitaji ya familia kama vile kulea watoto na kulipa kodi yapatikane. Ingawaje, iko mambo ambayo hawezi kuyafanya ya kujikosea heshima kama kupigwa picha akiwa uchi wa mnyama na kufanya ngono kwa njia isiyo ya kawaida.

Hawa wanawake wakati mwingine huwa baraka kwa jamii, kwani hata akisaidika yeye hufanya familia iwe na heshima sawa na iliyo na mme. Mambo mengine ambayo yanaweza kumfanya aambatane na umalaya ni kama mama au baba yake amekuwa katika kazi hiyo, ama laana katika familia.

**<u>Kutotosheka kingono</u>**

Kulingana na maumbile ya wanadamu, kuna watu ambao huwa na joto zaidi miilini mwao na huwa hawatosheki kwa haraka. Watu hawa wanaweza kuwa na heshima na wawe hawana shida yoyote katika kudumisha familia, lakini asipopatana na mwenye joto nyingi kama yeye, basi hilo laweza kuleta shida katika familia.

Hawa wanawake hutelekeza familia zao hata kama zina mali na mme anayewajibika. Wengine hufikia kiwango cha kujikosea heshima na kutafuta yeyote atakayemridhisha kingono. Jambo hili huchangia pakubwa kwa mahusiano ya wanawake au wanaume wa umri mkubwa na vijana wa umri mdogo, bila kujali maneno ya watazamaji.

Basi, wao ni hatari sana kwa kuwa, wanaweza hata kuwaua mabwana zao, ili wapate nafasi nzuri ya kupatana na mwanaume nje ya ndoa, awatimizie mahitaji yao na kuwaridhisha. ***Hii shida ikiwa kwa mwanaume, yeye humuwaza mwanamke mwingine japo wako pamoja na mkewe kitandani.*** Mtu kama huyo, hawezi kudumisha familia yake.

## <u>Vifo</u>

Katika maisha ya binadamu kuna njia kadhaa ambazo vifo hutokea, watu huwa, hawazifahamu wala huwa hawataki kuzijua. Baadhi ya hizo ni kama;

**Maumbile**

Kulingana na vile ambavyo kumekuwa na vifo vingi ulimwenguni, watu wengi wamechanganyikiwa, kwa sababu wameshindwa kutofautisha kati ya vifo vya kawaida na vile visivyo vya kawaida. Hapo awali, mababu zetu walikuwa wakiishi kwa miaka mingi kuliko watu wa nyakati hizi wanaofariki kiholela.

Ulimwenguni, kifo cha kawaida kimekuwa kikiwapata watu wachache sana, ukilinganisha na nyakati za zamani. Ni vyema kufahamu kuwa kifo cha kawaida ni kile cha uzeeni, bali sio cha magonjwa wala ajali zozote zile.

***Kwa ukoo, watu walipofanya makosa walijua kuwa, wangelipatwa na laana ambayo ingewaletea mikosi na vifo maishani mwao.*** Walijua vifo vya kawaida viliwapata wale waliojiepusha na makosa hayo. Hapo awali, watu walijaribu sana kuepukana na tabia ama vyakula vilivyokatazwa, kulingana na maagizo ya ukoo ndio wasiadhirike. Katika ulimwengu wa sasa, watu hawafahamu hatari za dhambi na hicho ndicho kiini cha vifo visivyoeleweka katika jamii.

**Makosa ya mtu binafsi**

Mtu anaweza kufa kwa sababu ya makosa aliyoyatenda yeye mwenyewe kulingana na lishe ama mienendo yake. Haya hufanyika kwa sababu, mwenendo huchangia pakubwa, mtu anapoyafuata mawazo yake mwenyewe. Inampasa mtu kujihadhali na vikundi anavyojiunga navyo, ili kuepukana na shida, na hatimaye, kifo.

Kama ilivyosemekana hapo awali, mtoto anapokua na kukomaa anaweza patana na laana. ***Hili huwapata watoto wa kiume, kwa sababu ya ukali wao na ujanja wa maisha***. Mambo haya hufanyika anapotafuta namna ya kuishi na baadaye kumwelekeza katika mauti. Sio jambo rahisi, kumtambua mtu aliye na laana. Ingawaje, yeye hutofautishwa kwa mwenendo na hata matamshi yake, kwa sababu huwa na ujasiri mwingine wakupindukia. Watu kama hao huwa hawana heshima kwa yeyote, kwani laana imewakubaza

**Makosa ya ulimwengu**

Viongozi wa ulimwengu waweza kumuasi Mungu, kwa kuongoza maisha ya wanadamu kwa njia zisizofaa kama; Nchi ikihisi kuwa na nguvu nyingi huwa inaanza kuzichokoza nchi zile zingine. Ili kuonyesha nguvu zake, nchi kama hizo hurusha makombora kwa zingine bila kujali iwapo jambo hilo litamwaga damu ya raia, wa nchi hizo. Ili ziogopwe zaidi, nchi hizo hulipua majengo makubwa na kambi za wanajeshi.

Viongozi wa madhehebu, viongozi wa dunia, na wasomaji ndio huaminika kama ngao ya raia, na wenye kudumisha maisha na heshima ya mwanadamu. ***Hawa viongozi wakati mwingine huwa hatari kwa maisha ya raia, kwani wanabadilika kulingana na mahali ama pahali walipo huo wakati***. Haya mambo mageni wakati mwingine huja kwa njia ya mapepo yale hufanya mmoja kigeugeu. Hao viongozi wanaweza kusaidia watu wengi, na vile vile kumaliza watu kwa wingi. Dunia imeshudhudia, madhehebu mengine na nchi zingine, vile maelfu ya watu wamekufa kupitia uongozi wao. Ni jambo la ajabu, viongozi wa Palestine na Israel, wanao heshima kubwa duniani, kukosa suluhu kuhusu kikundi cha Hamas. Suluhu wamepata ni kuonyesha ni nani ana nguvu na uungwaji mkono mkubwa duniani. ***Ukiwa unataka kuwa kiongozi bora, ni lazima uwe mtu, ndio uongezee hayo***

***mengine. Mtu huwa na mizizi ya kushika jambo geni, bila kupeperushwa kwa haraka***. Hali anaweza kufikiria umuhimu wa binadamu ili asife.

Baada ya Mungu, kutazama na kuona damu inavyomwagika, yeye hukasirika na kuachilia laana, kwa nchi zenye kujigamba na hivyo kuzifanya zipatwe na mambo mabaya. Hili laweza changia mwanadamu kufa kwa kosa lisilo lake. Ni vyema, kwa ulimwengu kuwaonya viongozi wapotovu, ili wasimkasirishe Mungu, bali wamfurahishe, kulinda na kuwatunza watu wake mahali popote ulimwenguni.

**Kupiganisha watu kwa misingi mbalimbali**

Kwa sababu ya ubinafsi, viongozi wa nchi hupiganisha raia, kwa njia za kisiasa ama za kikabila, ili wao wenyewe wafaulu katika mambo yao binafsi. Viongozi kama hao, humkasirisha Mungu na kumfanya aachilie laana ambayo huleta magumu ya ajabu, kama magonjwa yasiyopona na mambo mengine yanayoleta maafa.

Mungu alipoumba mwanadamu, alitaka wasaidiane, kwa mambo yote ya maendeleo ya maisha bila kubaguana, kwa misingi ya rangi, kidini wala kikabila. ***Basi, Mungu alitarajia kila mmoja achangie ili ulimwengu uendelee kwa pamoja.*** Lakini wakati mwingine, wanadamu husahau na kuwafanyia wengine matendo ya kinyama, huku wakiwatumia vibaya.

## Sababu za magonjwa

Watu huhangaika wakitafuta mwanzo wa masaibu yanayowakumba katika jamii. Wengine hata huenda kwa manabii ama waganga bila kukumbuka madai ya wazazi au ukoo. Wengine hutumia mamilioni ya pesa hospitalini kwa kutojua wangepata suluhu nyumbani. ***Masomo ni jambo la muhimu sana lakini, ni vyema mtu kuzingatia heshima, kwa wale waliomwelekeza hadi akafaulu***. Hata kama watu hao walikuwa na upunguvu wa hekima, na walikuwa na ukorofi ama ubinafsi, ilimpasa mmoja kuwapa heshima ya kutosha. Ili wazee wadumishe heshima na uadilifu katika jamii, walifahamu ya kwamba, watu walikuwa na tabia tofauti lakini, lazima wangeishi pamoja. Basi, wazee walijukumika kuwafunza watu namna ya kuishi pamoja bila kutengana.

Uzao ulikuwa ukifunzwa mambo yaliyoleta laana ama mikosi, kwa familia, kama vile;

- Kumwaga damu ya mtu asiye na hatia
- Kutusi ukoo na kutowaheshimu watu wazima
- Kutotii wazazi
- Kutoheshimu mjomba/ shangazi/ watu wa ukoo zao
- Kutoheshimu raslimali za watu.

Mambo mengine yaliongezwa na jamii zenyewe, ingawaje hayakuwa ya ukoo. Mengi yalikuwa ya kibinafsi, hivyo yaliharibu sura ya ukoo.

Ni manufaa makubwa kurekebisha utamaduni. Lakini wazee wafaa wapewe heshima ya kutosha, ili marekebisho hayo yaambatane na baraka kutoka kwao.

Jambo hili lafaa kutekelezwa na watu wenye hekima na heshima ya juu, ili wasitishe jamii, kwani utamaduni huo, ulikuwa ni kiwango cha mawazo yao. ***Hekima na heshima zaweza kufanya nyoyo zao kukubali kulingana na vile ulimwengu umekuwa na hata wawahimize ya kwamba, hakuna Mungu wa Milima, Mabonde, Mahali fulani, na Kabila fulani.***

Mungu yupo, kila pahali juu, chini na kwa kila mtu. Hapo awali, watu walifanya maombi yao pahali palipokuwa patulivu na pazuri kulingana na mazingira na mahali walipoishi. Hizi zote zilikuwa njia za kutuliza roho ya Mungu ingawa, kulikuwa na shida ya mawasiliano, kati ya ukoo na mwingine, ili kumtolea Mungu ibada kwa pamoja, kama jamii moja, ya ulimwengu. ***Watu waliishi kwa upendo ingawaje, hilo lilikuwa pendo la wenyewe kwa wenyewe, katika misingi ya kabila, dini au ukoo kulingana na kuonana na kushauriana kwao.***

## Sababu za ubakaji

Watu hushangaa sana wakati mtu mzima amejihusisha na kitendo cha kumbaka mtoto mdogo ama msichana, ambaye hajakomaa ili aweze kujivutia.

Mara nyingi, mwenye kubaka watoto au akina mama wazee, vilevile mwenye kushiriki ngono na wanyama yeye huwa kama mwendawazimu. Mwenye kubakwa huwa na kitu ama sababu ya kujivutia, lakini hawa hawana namna ya kufikiriwa, ama kutaminiwa. ***Kwa hivyo, ni lazima mwenye kufanya kitendo hicho awe na msukumo wa mapepo ili aweze kufanya mambo haya***. Kwa mfano mwenye kubaka awe amelaaniwa au awe mwendawazimu. Sababu nyingine inayochangia ni kama dhamiri ya kuvutia ya mtoto yule amekomaa zaidi kuliko mwili kwani mwili wa mwanamke huvutia mwanaume kwa ukomavu wa dhamiri ya mwili.

Kitendo cha ngono hutokana na msisimko wa mwili baada ya mmoja kuwaza yale yatakayotokea baadae. ***Hili hufanyika kwa yule aliyejawa na utu (ubinadamu), kwani binadamu huwa na hisia za kuleta na kuzima msisimko. Hizi hisia huzuia mmoja asimuwaze: - <u>Mtoto, mzee, mgonjwa, familia na mtu asiyejijua.</u>***

Mambo hayo humfanya mtoto anapozaliwa apelekwe kwa watu watakaombariki ili aepushwe na mapepo mabaya au mikosi ya maisha. Lakini mtoto hangeweza ondolewa mapepo kama wazazi wake wana laana, kwani lazima hio familia ingetimiza matakwa ya ukoo ili wabarikiwe.

Hapo ndipo mjomba alijukumika kumsaidia mtoto ikiwa ukoo ulikuwa na madai fulani

ambayo yalifaa kufanywa na baba ya mtoto yule lakini hakuweza kuwajibika ili aweze kusafishwa kitamaduni kulingana na makosa yake. ***Jamii mbalimbali, zilifanya mambo tofauti, ili mtu afanyiwe tambiko la kuondolewa laana ingawa katika jamii nyingi watu walipeana kitu au mnyama kama ishara ya kutubu.***

## Sababu za ndoto

Watu hujaribu kufikiria chanzo cha ndoto lakini, wengi hukosa jawabu. Watu wengine huenda kwa waganga na manabii, ila hukosa kufanikiwa na majibu ya kuaminika. Kila mmoja hutoa sababu anazozidhania, kuwa ni kweli. Hawa wote, mara nyingi humwacha mwanadamu akiwa na hamu ya kutambua ukweli.

***Ndoto huwa ni jambo ambalo hushtua ama hufurahisha, kwa sababu, huwa inaambatana na mawazo, ambayo hutokana na kuona, kusikia na kuwaza***. Ndoto humsumbua mtu, hasa akiwa katika miaka ya ujana, kwani ni miaka ya kuwaza makuu.

Wakati mtoto anakua, huwa anayaona mambo mbali mbali, mengine ya kumfurahisha na mengine ya kumshtua. Haya yote hujirudia anapolala, na wataalamu huwahimiza watu wasimgonge mtoto akiwa katika hali hii. Hili laweza kumfanya mtoto akate roho, kwani anaweza kuwa katika ndoto hatari, kwa mfano, kuanguka katika shimo.

Ndoto kwa wanadamu husababishwa na mambo yafuatayo;

- Ujumbe wa Mungu wa kuonya ama kuinua
- Ujumbe wa mapepo yale huwa kwa hewa.
- Ujumbe wa mwili – Ukiwa na kasoro, kama umechoka ama ukipata msisimko wa jambo kwa kuona ama kuhisi

Ndoto nyingi hutokana na ujumbe wa mwili, kwa sababu hayo huchangiwa na mambo ambayo hushtua, mawazo kwa kuona, kufikiria ama pia kuhisi. Ili mtu aweze kujua chanzo cha ndoto, ni lazima afikirie haya yote, yenye kuchangia. Lakini, baadhi ya manabii wakujituma (waongo) na waganga hutafsiri ndoto bila kufanya uchunguzi.

Ndoto zaweza kutokana na ujumbe wa mungu, ndio yale mungu anataka yamfikie mwanadamu, kwa njia ya manabii. Ndoto zingine, zaweza kuwa mungu mwenyewe anataka kukuonya ama za mafanikio yako. Ndoto zingine ni mapepo yalioko kwenye hewa za waliokufa. Haya mapepo huwa na madai, kulipisha na vurugu kwa walio hai. Ukoo ulihimiza mmoja awe mwangalifu na kumbembeleza mzazi, hasa, wakati wa uzee, hata kama mzazi alikuwa mbaya. Hili, lilikuwa ndio mwenye kufa, asiachilie mapepo yake, yenye ubaya wa aina yoyote.

## Matokeo ya baraka au laana

Baraka na laana ni mambo ambayo humfanyikia mwenye kulengwa. Baraka humpata mwenye kubarikiwa na huwa inamkinga kutokana na shida mbalimbali. ***Mtoto***

***abarikiwaye anaweza kutoka kwa jamii iliyo na umasikini, lakini, aweze kufikia kuwa kiongozi.*** Kwa mfano, ulimwengu ulishangazwa na Barrack Obama, aliye na mizizi ya kiafrika, alipoiongoza Marekani.

Kuna viongozi wengine, baada ya kuhangaisha na kumwaga damu ya raia wasio na hatia, walikufa wakiwa na mahangaiko makubwa na umaskini, kama aliyekuwa Rais wa Uganda Idi Amin Dada na wengineo wa nchi mbalimbali. Hili jambo la baraka lilichangia pakubwa kwa wazee wa ukoo kushauri uzao wao, ili uepukane na tabia mbaya kama kutoheshimu watu wazima na kulaghai. Kwa hivyo, ni vyema ulimwengu kuangalia uongozi kwa kina ili viongozi wasije wakaziletea nchi zao laana.

## Sababu ya ulevi

Ulevi huwa unasababishwa na mambo manne ambao yamejificha ndani ya binadamu mhusika.

1 – laana huashilia mapepo ya aina yote kwa muadhiriwa kiwango ya kwamba, yeye hujisahau na kufanya jambo lolote linalotokea. ***Baada ya mmoja kuadhiriwa, hupotewa na furaha, na kutafuta njia yeyote ya maisha. Mwadhiriwa hapo ndipo huingiwa na mawazo ya pombe, sigara, na vitu vingine vya kujifurahisha.***

2 – Mambo mengine hutokana na madai ya mahari, ama msemo wa wazazi ambao hufungulia mapepo njia na kuangamiza muadhiriwa. Kwa kiwango kikubwa. ***Mawazo ya mtu hudanganyika ya kwamba, kutoa mahari ni hasara, lakini, ndio msingi wa familia, kwani huletea watoto baraka za maisha.***

3 – Mwenedo wa mzazi ni jambo la muhimu sana kwa mtoto, kwani mtoto huenda akiiga tabia za mzazi, haswa kilicho katika damu ya mzazi, husaidia ama kuadhiri mtoto. Kulingana na utaalamu wa madaktari, humshauri mwenye mimba asitumie pombe, bangi, na hata dawa za kulevya. Kuna hata wanaume ambao wanaweza kuwa walevi wakupindukia na hao huadhiri uzazi wao kwa dhamiri.

4 – Ujana hufanya wanaopendana kupatwa na mawazo, ya kuwa pamoja wakati wote. Katika harakati hizo, wao hufanya mambo mengi pamoja na wakati mwingine huharibiana kimawazo. ***Ujana hukaa wakati mwingine kama fumbo, kwani hutajua utakuwa mtu wa aina gani, wa baraka ama wa laana.*** Mawazo ya ujana mara nyingi huwadanganya vile watakuwa pamoja, wakisahau vile wanafikiria itabadirishwa na maisha bila kujua. Hali hii ndio hufanya waungane wafurahie maisha wakidhania watakuwa pamoja kesho.

# SURA YA 10: UPOTOVU WA ULIMWENGU



Uchafuzi wa mazingira

Kutojali kwa viongozi wa ulimwengu hewa imechafuka kwa kiwango cha kuharibu mazingira. Jambo hili linafanyika siku baada ya siku, huku nchi zikilaumiana zenyewe. ***Ulimwengu umenyamaza huku vijana wakionyesha, kusema na kutenda mambo yaliyo na aibu katika mitandao ya kijamii bila kuwa na wasiwasi, ilhali wao ndio tegemeo la kesho.*** Zoezi hili limepea kizazi cha sasa uhuru wa kuharibu mawazo ya wadogo wao, kama vile kucheza densi wakiwa uchi na hata wengine kutamka maneno yasiyo na nidhamu katika mitandao.

Ulimwengu umekosa ushauri mwema kwa raia wake mpaka wanawachagua viongozi wasio wakamilifu. Hili hufanya raia wadhulumiwe kwa kiwango kikubwa, huku Ulimwengu ukikosasa kuuheshimu utawala wa utamaduni kama muigo wa kuboresha maisha ya mwanadamu. Ingawa kunafaa marekebisho ambayo yanastahili yafanyika, lakini kwa njia inayofaa, ili kuzingatia mambo muhimu katika maisha ya mwanadamu. ***Uongozi ulio ulimwenguni umepotosha vizazi vipya, kwani ulijitwika jukumu la kukosoa utawala wa utamanduni bila kuonyesha heshima kwa wazee wenye kuridhi utamaduni huo.*** Vile vile, viongozi wengi wa kidini na serikali, wamewafanya wazee kuonekana kama wasio na hekima na kusababisha vizazi vipya kutoonyesha heshima kwao.

Upotovu huu huchangia vizazi kutoshughulika na baraka ambazo hutoka kwa wazee, ingawaje ni muhimu maishani mwao. Katika maisha ya watoto, mzazi huwa kiungo muhimu sana, hata ingawaje sio mkamilifu. ***Mzazi anapokosolewa ni vyema mtu***

***kuzingatia hekima na heshima kwani ana uwezo wa kubariki au kulaani.*** Kutokana na kupuuzwa kwa utawala wa utamanduni, ulimwengu umekumbwa na changamoto la wanawake kutowaheshimu waume wao. Jambo hili linaonyesha kuwa, ulimwengu wa kisasa umempa mwanamke fursa ya kudhulumu mwanaume, kwani sheria nyingi zimebuniwa kumchunga mwanamke, hata kama ana makosa. Sheria hizo pia hutiliwa maanani haswa kwa mwanamke kinyume na inavyotumika kwa mwanaume. Jamii imepuuza utawala wa utamaduni kama vile mwanamke kutofunika uchi na kudhulumu mwanaume kimawazo. Dhuluma hii huchangia baadhi ya wanaume kuwa na hamu ya kushiriki mapenzi nje ya ndoa na wengine kubaka. Wengine hushikwa na kushtakiwa kwa kosa la ubakaji. Jambo hili limechangia kuongezeka kwa mimba zisizotarajiwa, magonjwa yanayotokana na kushiriki ngono, na kuongezaka kwa wafungwa katika jela.

Tatizo hili limechangia wanasayansi kutafuta mbinu za upangaji uzazi ili kuzuia magonjwa na mimba zisizotarajiwa. Hii bado ni dhana potovu ambayo, imechangia kuongezaka kwa tabia za kushiriki ngono za mapema kwa watoto na mapenzi nje ya ndoa, kwa watu wazima na hata kueneza magonjwa. ***Vile vile, binu za utangazaji wa matumizi na uuzaji wa mipira imesababisha kuwe na ongezeko la usherati.***

Upotovu huu, umeenea hadi katika vyuo vya msingi na vyuo vikuu. Kigezo hiki, kinachangia baadhi ya sarakasi nyingi zinazotokea katika shule, ikiwemo kujihushisha katika ukahaba na utumizi wa dawa za kulevya. Haya yote yalijidhihirisha vizuri wakati wa janga la corona (covid-19) lililoenea dunia nzima hadi kukatokea janga zingine kama vile, mimba za kiholela na vifo. Kulingana na utamaduni, kujihusisha na ngono kulitengewa wanandoa pekee, ili kupata kizazi kipya au hata njia ya kujifurahisha. Lakini kwa sasa, ulimwengu umeonyesha kuwa, ngono ni kama biashara au mchezo wa kawaida.

Hali kadhalika, ulimwengu umekwaza jinsia ya kiume kwani mwanamke ameumbwa na uvutio, ili mwanaume aweze kupendezwa naye na kujihusisha na tendo la ndoa, la sivyo, robo tatu ya wanadamu hawangekuwepo. Hata hivyo, uvutio huu wa maumbile huwa hauna matatizo, Kama vile kuvalia mavazi mabaya na kutembea uchi. ***Hayo ni mambo yanayohitaji kipimo kutoka kwa viongozi wa ulimwengu, ili kuzuia mawazo ya wanaume kuharibika na kudhuru wasio na hatia, na kuzuia magonjwa ya ngono.***

Kwa hivyo, ni vizuri viongozi wa ulimwengu kutambua hata tofauti za watu wa mataifa, na jamii mbalimbali na kuelewa ya kwamba hawafanani kwa mawazo wala maumbile, ili watu waweze kuishi kwa heshima na ustaarabu. Kila mmoja hutegemea mazingira ili aweze kufanya lolote. Ijapokuwa viongozi wa ulimwengu hawatilii maanani mambo hayo ili kuweza kuyalinganisha.

Ndio maana kuna tofauti ya kimaumbile kati ya mwanamke na mwanaume, ambayo ulimwengu haujaweza kufafanua. Naye binadamu, kwa ujeuri wake, hakushughulika kuelewa sababu ya muumbaji kuumba jinsia tofauti. ***Ili kizazi kiwe na msingi bora maishani, lazima baba na mama wahusike katika maisha yake, kwani kila mmoja huwa na jukumu lake kwa mtoto.***

Majukumu hayo ni kama yafuatayo;



*Ushirikiano wa wazazi katika ulezi*

**Mwanaume**

Mwanaume huwa na jukumu la kushughulikia mahitaji ya msingi kama chakula, na maisha ya baadaye ya mtoto kama vile elimu.

**Kushauri**

***Ushauri wa mwanaume huwa na himizo kali ambalo huingia katika mawazo ya watoto na kuwaepusha katika majaribu ya maisha.*** Ushauri kwa watoto huwawezesha kujenga uhusiano mzuri na wenzao na kujitenga na yale mabaya katika maisha yao. Mwanaume hushauri jamii nzima, hasa wale waliokomaa na kuelewa uhusiano wa familia yake na ukoo.

**Kuonya**

***Mwanaume amepewa ubunifu wa kuweza kumuonya mtoto, kwa kumtia woga, ili kumzuia kutenda mabaya.*** Woga huu, husaidia mtoto kuzingatia mienendo yake, haswa akikumbuka onyo la baba yake.

**Kukinga**

Mwanaume anaweza kufia familia yake kwa sababu yeye hufanya lolote ili aikinge kutokana na hatari zozote. Ujasiri na ubunifu wa wanaume husaidia kuhakikisha familia zao ziko na ulinzi wa kutosha. Mtoto hufahamu ujasiri wa baba yake katika jamii, jambo ambalo hukuza heshima kati ya mtoto na mzazi.

**Mwanamke**



*Mama na watoto*

Mwanamke huwa na mambo manne kwa mtoto, ambaye hufanya mama awe na uhusiano mkubwa na yeye kuliko baba. Nazo ni:

***Kulisha***

***Kulisha mototo hufanya uhusiano mkubwa kwani, akili na mwili hukuwa pamoja na wakati wote wako uso kwa uso.*** Wakati mtoto anakuwa huwa anaweka kila jambo analoliona kwa macho na kufanya awe vile atakuwa maishani, na ndio sababu mara nyingi anakumbuka mama yake.

***Kumbebeleza***

Hili jambo, hufanya mtoto ajisikie hayuko hatarini kwani haoni wala hasikii ili ajue ako wapi. Kubebeleza hufanya dhamiri zake zikubali mazingira alioomo mpaka kimawazo. Kwa hivyo, ndio kukubali mikono ambayo humshika na kumbebeleza.

***Kutunza***

Kutuza husaidia dhamili na mawazo ya mtoto kujihisi amekubalika ulimwenguni. Akina mama wako na roho ya kutunza watoto.

***Kukinga***

Kulingana na maumbile ya mwanamke, anaweza kumlinda na kumtetea mtoto iwapo ako katika hali ya hatari kwa sababu ya pendo lake. Pia, shida ya mwanamke ana huruma nyingi hadi kutokubali, kuwa mtoto wake anaweza fanya jambo mbaya.

Kwa hivyo, majukumu haya yanaweza kutekelezwa na yeyote ingawa kila upande umepewa na Mungu roho ya kufanya mambo hayo kwa urahisi bila kukwazika kiakili. Basi, ulimwengu haufai kuwapotosha wanawake ya kuwa wanadharauliwa na wanaume, bali ni vile dunia ilivyo kuwa na ubinafsi na giza. Ubinafsi wa mwanandamu uliweza kumfanya awe na fikira za kumtawala mwenzake kimabavu na hata kusababisha vita, kama vile ilishuhudiwa katika nchi za Nigeria, Somalia, Kenya, na zingine.

# SURA YA 11: VITA VYA NIGERIA



*Wanajeshi wakikomesha vita Nigeria*

Zaidi ya watu wapatao milioni moja (1,000,000) waliuawa kutokana na vita vya Biafra viliyodumu kwa takribani miezi therathini (30). Athari zake bado zingalipo hadi wakati huu, ingawa kila kitu hakipo kama inavyotegemewa miaka hamsini tangu tamati ya vita hivyo. Uchenna Chikwendu alizungumza kwa kina mambo muhimu kuhusiana na vita vya Biafra. Chikwendu, aliyekuwa mwenye umri wa miaka sitina na saba (67), aliishi katika maeneo ya Enugu katika mji mkuu wa jimbo lenye jina sawa mashariki mwa Nigeria ambalo lilikuwa sehemu ya taifa lililojitangazia uhuru wake la Biafra. Wakati wa vita hivyo vya Biafra vilivyoanza mwezi wa Julai katika mwaka wa 1967 na kumalizika katika mwezi wa Januari tarehe 15, mwaka wa 1970, Chikwendu alikuwa katika umri wa makamu.

Maneno ya Chikwendu yaliashiria ya kwamba, "***Tulikuwa tunatembea mara kwa mara. Hakukuwa na magari. Yeyote aliyekuwa na gari lake ilibidi alifiche ili wanajeshi wasije kulichukua. Haikuwa rahisi, tulikuwa tunatembea kwa miguu. Tulienda soko saa tisa alfajiri na kufika mwendo wa saa tano. Tulifanya ununuzi wetu kwa haraka na tukiwa njiani tukirudi nyumbani, tulikuwa tunachukua tahadhari kubwa, ili tusionekane***."

Vita vya Biafra vilipata umaarufu zaidi katika nchi ya Nigeria kama vile Uchenna Chikwendu alivyoyosimulia kwa kina, kuhusu uzoefu wake kwenye hivi vita. Nigeria ni taifa lenye makabila yaliyozidi jumla ya 250, lililojinyakulia uhuru kutoka Uingereza mnamo mwaka wa 1960, wakati ambapo, hili taifa likiwa na jumla ya watu milioni 45. Katika wakati huo, ni dhahiri ya kwamba maeneo ya kaskazini yalikuwa na jamii za Wahausa pamoja na Fulani, maeneo ya kusini-magharibi waliishi Wayoruba na vile vile kusini-mashariki waliishi jamii ya Igbo. Harakati za mapambano ya kuwania madaraka na rasilimali yakazuka. Hii inamaanisha kwamba, ubinafsi wa watu fulani kunyakua

raslimali kulichangia pakubwa kuzuka kwa vita vya Biafra.

Mapinduzi mawili yaliyohusisha wanajeshi yalifuatana katika mwaka wa 1966: Kwanza, Majenerali ambao waliongozwa na Johnson Aguiyi-Ironsi, aliyetoka katika jamii ya Igbo walimpindua Abubakari Tafawa Balewa kutoka kwa mamlaka yake ya waziri mkuu wa eneo la kaskazini. Miezi sita baadaye, mapinduzi mengine yalifuatia ambapo majenerali hasa kutoka maeneo ya kaskazini walishiriki. Baada ya machafuko makubwa ya kikabila, Chukwuemeka Odumenwu Okukwu, ambaye alikuwa ni gavana wa kijeshi wa jimbo hilo la kusini-mashariki, alilitangaza jimbo hilo kuwa taifa huru mnamo mwezi wa Mei, tarehe 30, mwaka wa 1967.

## Nigeria yasalia kuwa taifa lililogawanyika

Kilichofuata hapo baadaye ni vita vikali. Inakadiriwa kwamba kati ya watu 500,000 na 3,000,000 walifariki kufuatia hivi vita. Kulingana na profesa mmoja wa siasa linganishi katika chuo kikuu cha aliyejulikana kama Ibadan Eghosa Osaghae, sababu za hivi vita haijabainika mpaka leo. Kulingana na matamshi ya Profesa Osaghae "***Watu huwa na mafikira ya kwamba sehemu za kusini-mashariki ndizo zilizo katika hali ngumu na udhaifu zaidi kimamlaka. Na hilo linaweza kuwa linatokana na athari za vita vya Biafra. Lakini hayo yote ni dhana tu.***"

# SURA YA 12: VITA VYA SOMALIA



*Vita katika nchi ya Somalia*

Watoto katika taifa la Somalia walishiriki katika vita kama wanajeshi. Hili ni suala muhimu ambalo linaendelea mpaka kwa mwaka huu wa 2024. Katika taifa la Somalia, kulikuwa kumezuka vita vingi pamoja na migogoro ya aina mbalimbali ambayo imehusisha watoto wanajeshi. Katika vita vijulikanavyo kama "***Vita vya Mogadishu***", vikundi vyote ambavyo vilihusika katika vita hivyo vilitumia watoto kama wanajeshi. Hili ni jambo la kuhuzunisha, kwani ni dhahiri kwamba, dunia imekosa heshima kwa watoto, ambao wanafaa kuwa tegemeo la kesho kama viongozi. Baadhi ya vikundi hivyo ni kama vile: "***Umoja wa Mahakama za Kiislamu***", "***Muungano wa Marejesho ya Amani na Mapambano Dhidi ya Ugaidi***", na pia vikosi vya usalama vya "***Serikali ya Mpito ya Shirikisho***".

Kikundi hiki kijulikanacho kama "***Serikali ya Mpito ya Shirikisho***" kimeorodheshwa na Umoja wa Mataifa, kama mojawapo ya vikundi vikuu, ambavyo vinawaajiri na pia kuwatumia watoto katika jeshi na pia katika vikosi vyao vya usalama, jambo ambalo linakiuka haki za kibinadamu na za watoto. Inafaa kukumbukwa na kufahamika, ya kwamba Umoja wa Ulaya na vile vile taifa la Marekani, kwa wakati huu ni wasaidizi tajika katika vikosi vya kulinda usalama vya "***Serikali ya Mpito ya Shirikisho***" katika taifa la Somalia. Vile vile, taifa kuu la Marekani limefidia mishahara inayohitajika katika vikosi vya kulinda usalama vya "***Serikali ya Mpito ya Shirikisho***". Hii inamaanisha ya kwamba, taifa la Marekani ni msaidizi maalum wa serikali ambayo inakiuka "***Sheria ya Kuzuia Wanajeshi Watoto***".

Ni muhimu kufahamu ya kwamba, kikundi cha kigaidi maarufu kwa jina la Al-Shabaab, ambacho kwa wakati huu, kinapigana vita katika taifa la Somalia kwa madhumuni ya

kuunda Taifa la Kiislamu, ni kikundi mbadala ambacho kinawaajiri na kutumia watoto katika vita wakitumika katika vitengo vya kijeshi katika vita vyao. Hii pia ni dalili ya kuenea kwa maovu katika sehemu mbalimbali humu duniani, bila kujali masilahi ya wanyonge. Hali hii pia inadhihirisha kiwango cha kuenea kwa maovu katika sehemu tofauti hapa duniani.

# SURA YA 13: VURUGU BAADA YA UCHAGUZI NCHINI KENYA



*Vurugu baada ya uchaguzi*

Kenya ilipata uhuru mwaka wa elfu moja mia kenda sitini na tatu (1963), na ikapata kiongozi wa kwanza, Mzee Jomo Kenyatta wa chama cha KANU [*Kenya African Natonal Union]*. Aliliongoza taifa hadi mwaka wa elfu moja mia tisa sabini na nane (1978), ambapo alifariki, kwa kuugua kwa muda mfupi. Baada ya kifo chake, aliyekuwa naibu Rais na msaidizi wake Bwana Daniel Toroitich Arap Moi alichukua hatamu za uongozi hadi alipostaafu katika mwaka wa elfu mbili na mbili.

Hatimaye, katika mwaka huo huo wa 2002, taifa liliandaa uchaguzi, ambapo Bwana Mwai Kibaki aliteuliwa kuwa Rais wa tatu kupitia chama cha NARC (*National Rainbow Alliance Coalition*), katika jamuhuri ya Kenya. Aliiongoza nchi kwa ustadi hadi mwaka wa 2007, ambapo alianza kukabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Raila Odinga, ambaye alikuwa wa chama cha ODM (*Orange Democratic Movement).* Raila aliteuliwa kuwa muwaniaji wa urais kupitia chama hicho, baada ya kupita chaguzi za mchujo. Mwai Kibaki alikuwa ameungwa mkono na vyama kadhaa, ambavyo viliunda muungano wa PNU (Party of *National Unity).*

Uchaguzi mkuu uliandaliwa na iliyokuwa tume ya uchaguzi wakati huo (ECK). Rais Mwai Kibaki alitangazwa kuwa mshindi kwa muhula wa pili na aliyekuwa mwenyekiti wakati huo Bwana Samwel Kivuitu.  Hii ni baaada ya kupata upinzani mkali kutoka kwa chama cha ODM chake Raila Odinga kwa umaarufu “Baba”.

Ushindi wake Kibaki ulikabiliwa na tetesi kutoka kwa mshindani wake wa karibu Bwana Raila Odinga, kwani aliyakataa matokeo ya uchaguzi na kudai kuibiwa kura. Alijitetea kwamba ndiye aliyekuwa mshindi na kwamba alipigwa chenga, katika zoezi hilo na aliyekuwa mwenyekiti wa tume ya uchaguzi Bwana Samuel Kivuitu.

Bwana Raila Odinga aliitisha mikutano ya maandamano ya kupinga ushindi wa Kibaki. Mapambano, vurugu na ghasia za kila aina zikashuhudiwa katika sehemu nyingi za nchi. Mamia ya watu waliaga dunia na maelfu wakabaki wamejeruhiwa kwa makali ya vita. Wananchi wengi walichomewa makaazi yao. Biashara na kazi nyingi hazikuwa na budi kusitishwa. Wanawake wengi waliachwa wakiwa wajane na watoto wakabaki mayatima. Vita vya kikabila vilihangaisha uchumi wa nchi na kuisababisha nchi ya Kenya kuwa katika mtazamo wa dunia nzima. Biashara ambazo hufanywa ughaibuni pia ziliathirika pakubwa haswa katika sehemu ya utalii, kwani wengi walihofia kuyapoteza maisha yao iwapo wangeizuru nchi ya Kenya wakati huo.

Juhudi za kuleta amani zilianzishwa na viongozi kutoka nchi mbalimbali. Miongoni mwao ni aliyekuwa Rais wa Tanzania Bwana Benjamin Mkapa, Umoja wa mataifa (UN) ulimtuma aliyekuwa katibu mkuu mstaafu Bwana Kofi Annan. Lengo lao lilikuwa kuleta uwiano kati ya mheshimiwa Raila Odinga kiongozi wa chama cha upinzani(ODM), na aliyekuwa rais na kiongozi wa chama cha PNU, Bwana  Mwai kibaki. Mazungumzo ya wazi yalifanywa. Viongozi hawa wawili walikubaliana kuunda serikali ya mseto na ndiposa amani na utulivu ukarejea.

# SURA YA 14: SAFARI YA KISIASA YA UHURU KENYATTA



*Raisi Uhuru Muigai Kenyatta*

Bwana Uhuru Muigai Kenyatta alizaliwa Oktoba 26 mwaka 1961, akiwa mwana wa rais wa kwanza Mzee Jomo Kenyatta na mke wake wa nne Mama Ngina Kenyatta. Alilelewa katika maisha ya ukwasi na kusomea katika shule za kifahari, zikiwemo shule ya St Mary's, Nairobi. Alipomaliza masomo ya shule ya upili, alifanya kazi kwa muda kama karani katika benki ya Kenya Commercial Bank (KCB), tawi la "Kipande House", Nairobi kabla ya kuelekea Chuo kikuu cha Amherst, katika jimbo la Massachusetts Marekani, ambapo alisomea na kuhitimu katika shahada ya sayansi ya siasa. Baada ya kurejea Kenya, alijishughulisha na biashara hasa kilimo cha mboga na matunda. Alianza kuchangia katika usimamizi wa biashara za familia. Kenyatta aliingia katika siasa mwaka wa 1990. Katika mwaka wa 1997, aliteuliwa mwenyekiti wa tawi la chama tawala cha wakati huo Kenya African National Union (KANU), katika eneo lake la Gatundu. Aliwania ubunge katika eneo bunge la Gatundu Kusini katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1997 kupitia chama cha KANU lakini, akashindwa na Moses Muihia wa chama cha Democratic Party (DP) kilichokuwa cha Mwai Kibaki. Rais mstaafu Moi alimkuza Uhuru Kenyatta kisiasa. Wengi walitarajia kuwa angeshinda lakini, baada ya kushindwa, Uhuru alighadhabika sana na hata kuahidi kuiasi siasa. Wengi waliona hatua ya Moi kama ya kumtayarisha Uhuru kwa mambo makubwa katika siku za baadaye. Mara moja akarejea katika biashara za familia yake ambazo, zinajumuisha hoteli tano mashuhuri, kampuni za vifaa vya ndege na kilimo na biashara. Hakujua kuwa Moi bado alikuwa na mpango naye kutaka kumpeleka katika ngazi za juu kisiasa. Kwa miaka miwili, hakusikika sana hadi mwaka wa 1999 alipoteuliwa kuwa mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Kenya (KTB) na Rais Daniel Moi. Mwaka uliofuata, Bwana Moi alimteua kuwa mwenyekiti wa Kamati ya Kuratibu Juhudi za Kukabiliana na Majanga. Mwaka 2001, mwezi Oktoba, aliteuliwa na Moi kuwa mbunge maalum



*Raisi wa pili wa kenya – Daniel Moi*

Rais Moi kisha alimteua kuwa waziri wa serikali za mitaa mwezi mmoja baadaye. Mwaka 2002, alichaguliwa kuwa mmoja wa wenyekiti wanne wa chama cha Kanu, na baadaye akaidhinishwa kugombea urais na chama hicho. Katika uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 27 Desemba, 2002, Kenyatta alishindwa na mgombeaji wa upinzani Mwai Kibaki aliyepata asilimia 62 za kura, Bw Kenyatta naye akapata asilimia 31. Wakati huo, Kenyatta alipuuziliwa mbali kama 'mradi wa Moi', na wengi hawakutarajia kwamba nyota yake kisiasa ingeendelea kung'aa.

Kwa muda, alitaka kuonyesha watu kuwa, yeye anaweza kujitegemea mwenyewe wala sio kibaraka cha Moi kama wengi walivyokuwa wanasema. Katika bunge jipya alikuwa kiongozi wa upinzani lakini, alipata pia upinzani ndani ya chama hasa kutoka kwa kigogo wa chama cha KANU Nicholas Biwott pamoja, na wanasiasa kutoka Bonde la Ufa. Januari 2005 alimshinda Biwott walipogombea uwenyekiti wa chama hicho na hapo Biwott akaondoka chamani na kuunda chama chake cha New Kanu. Katika kura maalumu ya wananchi kuhusu katiba mpya Uhuru aliungana na viongozi wengine, katika kambi ya Chungwa wakiwemo Bwana Raila Odinga na Kalonzo Musyoka na kufanikiwa kuushinda upande wa Serikali. Viongozi walioipinga rasimu ya katiba iliyokuwa imependekezwa wakati huo waliungana na kuunda chama cha Orange Democratic Movement (ODM). Mipango yake ya kushiriki katika harakati za ODM zilipingwa vikali ndani ya chama kwa sababu viongozi wengine wa KANU pamoja na rais mstaafu Moi aliogopa kuwa chama hicho cha uhuru kingeangamia. Novemba 2006, Biwott alirudia jaribio la kumpindua Uhuru kwa kuitisha mkutano wa Kanu mjini Mombasa bila idhini ya mwenyekiti wala kamati ya chama. Hapo alichaguliwa kuwa mweyekiti mpya. Kwa msaada wa serikali, Biwott alifaulu kuandikisha kamati yake kama kiongozi rasmi, hivyo kumwondoa Uhuru katika nafasi ya kiongozi wa upinzani bungeni. Uhuru aliupinga uchaguzi wa Biwott na Mahakama Kuu ya Mombasa ikabatilisha kura ya tarehe 29 Desemba 2006, na baadaye uamuzi huo ukathibitishwa Juni 2007, na kuamua kwamba hakukuwa na ushahidi wowote kuthibitisha madai ya Bw Biwott na wenzake kwamba Bw Kenyatta alikuwa amehamia

chama kingine. Juni 2007, Uhuru alionyesha wazi kwamba alitaka kuacha ushirikiano wa ODM kwa kutopeleka jina lake kati ya wagombea wa urais upande wa ODM. Badala yake, alieleza kuwa atampigania rais Kibaki, ili achaguliwe tena. Alisema kuwa hana nia ya kugombea urais ikiwa hana uhakika kuwa atashinda. Kufuatia uchaguzi uliokumbwa na utata, Kibaki alitawazwa kama rais licha ya utata huo. Kibaki naye alimteua Uhuru kama waziri wa serikali za mitaa na baada ya mapatano kati ya Kibaki na Odinga, Uhuru aliteuliwa kama naibu waziri mkuu ikiwa ni sehemu ya mpango wa kugawana mamlaka. Aliondolewa kuwa waziri wa serikali za mitaa na kuteuliwa waziri wa fedha mwaka 2009.

## Kuchaguliwa kwa rais mwaka 2013

Safari yake ya kisiasa ilichukua mwelekeo mpya Desemba 15, 2010 alipotajwa na mahakama ya ICC kama mmoja wa wahusika wakuu katika ghasia za baada ya uchaguzi. Alituhumiwa kupanga na kufadhili ghasia katika maeneo ya Naivasha na Nakuru. Uchaguzi wa mwaka 2013 ulipokaribia, alijitosa kwenye kinyang'anyiro cha urais kupitia chama cha The National Alliance (TNA) ambapo alishirikiana na William Ruto wa chama cha United Republican Party (URP).

## Utawala wa Uhuru Kenyatta

Uhuru Muigai Kenyatta, ambaye ni mwanawe Raisi wa kwanza nchini Kenya, alichaguliwa raisi baada ya kustaafu kwa raisi wa tatu wa Kenya bwana Mwai Kibaki.



*Raisi wa tatu wa kenya – Mwai Kibaki*

Uhuru alimshinda mpizani wake Raila Odinga kwa asilimia 50.07 ya kura kwa mujibu wa matokeo yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi na hivyo kuepuka marudio ya uchaguzi. Ushidi huu wa kura milioni 6.13 kulinganishwa na kura milioni 5.3 alizopata mpinzani wake. Takwimu za tume ya uchaguzi zilionyesha kwamba Uhuru Kenyatta alishinda kura 6,173,433 kati ya jumla ya kura 12,338,667 zilizopigwa. Odinga amejipatia kura 5,340,546. Raila hakuridhika na matokeo haya na ikambidi kupinga kwa kuwasilisha kesi katika mahakama kuu, ambapo Mahakama ilimthibitisha Uhuru Muigai Kenyatta kuwa mshindi halali wa uchaguzi wa urais.

Rais Uhuru Muigai Kenyatta aliibuka kuwa rais wa umri mdogo zaidi kuwahi kuongoza

nchi ya Kenya aliposhinda uchaguzi mkuu wa Machi mwaka 2013 akiwa na mgombea mwenza Dkt. William Samoei Ruto. Mwaka 2017 wakati wa uchaguzi mkuu, hali ilikuwa tofauti sana lakini walifanikiwa kushinda urais kwa kupata kura 8,203,290 ambayo ni sawa na asilimia 54.27 ya kura zilizopigwa wakati wa uchaguzi wa tarehe 8 Agosti. Lakini Mahakama ya Juu ilitupilia mbali uchaguzi huo na kusema ulijawa na kasoro nyingi. Mahakama hiyo ikiongozwa na Jaji Mkuu David Maraga iliagiza uchaguzi mpya ufanyike.

Wawili hao walijipigia debe tena kwa wananchi kama viongozi wa kisasa, vijana wa kuleta mabadiliko - kwa kifupi viongozi wa kidijitali. Waliwabatiza wapinzani wao kuwa wazee waliosimamia mambo ya zamani - analogi. Kwa bahati, wawili hao waliweza kushinda uchaguzi, lakini mnamo mwaka wa 2017, mambo yalibadilika. Rais Kenyatta alitetea kuchaguliwa tena, kwa msingi wa aliyoamini alikuwa ameyatimiza na serikali yake kwa miaka minne na miezi kadhaa ambayo alikuwa uongozini. Chini ya uongozi wake, mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kati ya Mombasa na Nairobi ulikamilishwa na wananchi waliweza kusafiri kwa masaa manne safari ambayo awali ilikuwa ikichukua masaa zaidi ya nane. Kwa kujaribu kutimiza sera zake kama kiongozi wa kidijitali, serikali yake ilijaribu kutimiza ahadi za kuwapa wanafunzi wa shule za msingi vipakatalishi. Mradi huo ulikumbwa na changamoto si haba. Awali, ahadi ilikuwa kuwapa watoto wa darasa la kwanza vipakatalishi, na baadaye kila watoto wanaojiunga na shule ya msingi kila mwaka. Mwishowe wanafunzi wote katika shule za msingi kuwa nazo. Mpango huo ulibadilishwa na badala yake wanafunzi walipewa tableti. Serikali ya Bwana Kenyatta pia ilizindua vituo maalum vya kutoa huduma za serikali kwa jumla sehemu moja.

## Vituo vya Huduma [Huduma Centre]

Kupitia vituo hivyo, Wakenya waliweza kupata na kulipia huduma kama vile ulipaji kodi, vitambulisho, leseni za udereva, huduma ya bima ya taifa ya hospitali na kadhalika.




*Jengo la Huduma za serikali (Huduma Center)*

Serikali yake pia ilianzisha tovuti ya kutumiwa na wananchi kufuatilia utekelezaji wa miradi iliyoahidiwa na serikali. Aidha, kulikuwa na tovuti ya kupiga ripoti mara moja kuhusu visa vya ulaji rushwa moja kwa moja hadi kwa rais. Wakosoaji wake hata hivyo, walisema mengi kati ya miradi hiyo ni ya kujipendekeza kwa wananchi lakini haijaimarisha uwazi, na pia haijasaidia kupiga kwa vita ufisadi. Bw Kenyatta alipata wafuasi wengi sana kwenye mtandao wa Facebook na Twitter, huwa mara kwa mara wanafuata mitindo inayovuma mtandaoni. Mfano aliwahi kucheza dansi ya dab, ilipokuwa inavuma. Wakati wa kampeni, alifanya vikao viwili moja kwa moja kwenye Facebook kupokea na kujibu maswali ya wananchi.

Kenyatta bado alikabiliwa na mashtaka ya uhalifu dhidi ya ubinaadamu, kufuatia uchaguzi wa Kenya wa mwaka 2007 uliozusha umwagaji damu wa kikabila. Kufuatia kutangazwa kwake na Tume ya Uchaguzi kuwa mshindi wa uchaguzi huo, Kenya ilikuwa nchi ya pili ya Afrika baada ya Sudan kuwa na rais aliyeko madarakani aliyekabiliwa na mashataka, katika mahakama ya kimataifa, ya uhalifu ya ICC yenye makao yake kule “The Hague” nchini Uholanzi.



*Uhuru Kenyatta katika Hague inchini Uholanzi (The Hague)*

Marekani na mataifa mengine ya magharibi yalisema, kabla ya kufanyika kwa uchaguzi huo kwamba, ushindi wa Kenyatta ungefanya uhusiano wa kidiplomasia na nchi hiyo kuwa mgumu, ambayo ni mshirika mkuu katika vita dhidi ya wanamgambo wa itikadi kali za Kiislamu katika kanda hiyo. Mwanadiplomasia mmoja wa mataifa ya Magharibi alisema kwamba, halitakuwa tatizo iwapo Kenyatta atakubali kushirikiana na mahakama ya ICC na kwamba wangeheshimu uamuzi wa wapiga kura walio wengi nchini Kenya.

Uhusiano kati ya serikali za nchi za Magharibi na Kenya chini ya utawala wa Kenyatta

uliambatana na jinsi Kenyatta na naibu wake William Ruto ambaye pia walishtakiwa katika mahakama ya kimataifa ya uhalifu ya ICC walivyotoa ushirikiano wao, katika mahakama hiyo. Wote wawili, Kenyatta na Ruto, walijitahidi katika harakati za kuondolewa mashtaka. Kwanza, Kenyatta angezima vijembe vya Odinga wakati wa kampeni, kwa kuliongoza taifa kupitia mtandao wa „Skype‟ kutoka The Hague makao makuu ya mahakama ya ICC. Hali ya wasiwasi ilitanda nchini Kenya na mji wa Kisumu uliongoza ukiwa ndio mji wenye wafuasi wengi wa mpizani wa Kenyatta, Raila Odinga ambaye alikuwa nyuma ya Kenyatta baada ya kupata asilimia 43.28 ya kura. Wafuasi wake walikuwa wakipiga mayowe kwamba "bila Raila hakuna amani" huku vikosi vya usalama vikijishughulisha na mapambano kule Kisumu ambapo, kulizuka ghasia kufuatia uchaguzi wa mwaka 2007.

Mshauri wa kisiasa wa Odinga, Salim Lone, alimshauri Raila kutoyakubali matokeo hayo na badala yake awasilishe kesi ya kupinga matokeo mahakamani. Kambi ya Odinga ilidai kwamba, wakati kura zilipokuwa zikihesabiwa kulikuwa na kasoro kubwa sana na kutaka zoezi hilo kusitishwa. Nchi nyingi ziliamini kwamba, Kenya ni mojawapo ya mataifa yenye demokrasia imara barani Afrika, hata hivyo vurugu za baada ya uchaguzi zilisababisha vifo vya zaidi ya watu 1,200 mwaka huo wa 2007.

Wakenya wengi walitumai sana kuepuka marudio ya vurugu za baada ya uchaguzi, kama zile za mwaka 2007 ambazo ziliziangamiza uchumi wa nchi. Viongozi wa kidini katika mji wa Kisumu na sehemu nyinginezo za magharibi mwa Kenya zilizoathirika, walichukua juhudi za kuleta amani na utulivu. Waangalizi wa kimataifa kwa kiasi kikubwa walitaka uchaguzi na zoezi la kuhesabu kura lifanyike kwa uwazi na tume ya uchaguzi kuwajibika.

Wanasiasa wengi hutegemea makundi yao ya kikabila katika taifa ambapo, utiifu wa kikabila mara nyingi umekuwa juu kuliko kuzingatia sera za vyama wakati wa kupiga kura. Wakenya wengi waliamini ya kwamba uchaguzi huu ulikuwa na uwazi zaidi. Idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura ni asilimia 86 kati ya watu milioni 14.3 waliostahiki kupiga kura.

Baada ya kesi kuwasilishwa kotini, upande wa upinzani ulishindwa kutoa ushahidi wa kutosha kudhibitisha madai yao. Mahakama ilitupilia mbali ushahidi wa mamia ya kurasa uliowasilishwa na Odinga kuongeza udhibitisho wa tuhuma za kuwepo kwa mapungufu, ingawa hiyo ilikuwa sehemu ya ushahidi uliowasilishwa. Mahakama hiyo iliamuru kuwa kura zihesabiwe upya katika vituo 22, ikiwa ni sehemu ya jumla ya vituo 32,000 vya kupigia kura nchi nzima. Kenyatta, alitangazwa mshindi Machi 9. Odinga aliwasihi wafuasi wake kusalia watulivu wanaposubiri uamuzi huo wa mahakama, na akaahidi kuuheshimu uamuzi huo. Lakini bado nchi yote ilikuwa imejawa na msukosuko wa kiuchumi na siasa ya ukabila.

Baada ya miaka miwili, Raisi Kenyatta alimualika Raila Odinga katika ikulu yake na wakakubaliana kusitisha tofauti zao, na kufanya kazi kwa pamoja. Uhusiano huu ulileta hali ya utulivu na amani nchini Kenya na kumwezesha Raisi Kenyatta kutekeleza majukumu yake. Raisi Kenyatta na Raila Odinga walitoa uamuzi wa kubadilisha sheria kupitia kwa makubaliano yaliyojulikana kama "BBI" (Building Bridges Initiative). Baada ya mazungumzo ya miezi kadhaa kati ya wanachama wa BBI, makubaliaono yaliwasilishwa bungeni na kupitishwa kuwa sheria. Kesi iliibuliwa na kuwasilishwa katika mahakama ya upeo nchini ambapo, jopo hili la BBI lilitupiliwa mbali kwa kuwa, kinyume cha sheria. Mahakama ilitoa uamuzi ya kwamba, rais Uhuru Kenyatta alikiuka katiba katika kuanzisha mchakato wa BBI. Kulingana na ripoti ya Mahakama, Rais Uhuru Kenyatta alitumia nguvu zaidi ya uwezo wake kikatiba alipoanzisha mchakato wa kubadilisha katiba kupitia mpango wa BBI. Katika uamuzi mkali dhidi ya mchakato huo wa amani nchini Kenya, majaji watano walisema kwamba rais Uhuru Kenyatta alifanya makosa kadhaa ya kikatiba wakati alipokuwa akianzisha mpango huo wa mabadiliko ya kikatiba.



*Rais Uhuru kenyatta na waziri mkuu Raila Odinga wasalimiana[Handshake]*

Mahakama ilitoa uamuzi kwamba, jopo la wanachama 14 lililobuniwa kuongoza mchakato huo lilikuwa kinyume cha sheria. Majaji hao walisema kwamba, rais alifanya makosa ya kisheria katika kujaribu kubadili katiba, njia ambayo hana uwezo kuitumia. Raisi alipaswa kutumia bunge kupitia mwanasheria mkuu kuamua kuhusu mabadiliko yaliyohitajika. Mahakama ilisema kwamba hakuna njia nyingine ya kubadili katiba isipokuwa kupitia bunge ama kura ya maoni. Waliutaja mchakato wote wa BBI, kuwa ulisimamiwa na rais badala ya kusimamiwa na bunge ama raia. Rais hawezi kuanzisha mchakato wa kubadilisha katiba, na BBI imegubikwa na mgongano wa maslahi.

Kwa wale waliodai kwamba, rais Uhuru Kenyatta alikuwa akichukua hatua hiyo kukuza umoja wa kitaifa, mahakama ilisema kwamba hoja hiyo inamsaliti na ukweli ni kwamba, kamati simamizi ya BBI iliundwa na rais na kumuwajibikia yeye.

Mchakato wote wa BBI ulikuwa mpango uliohusisha rais Uhuru kenyatta, wakishirikiana na rafiki yake aliyekuwa mpizani wake mkuu katika uchaguzi wa 2013, na aliyeibuka kama kinara wa chama cha upinzani, Raila Amolo Odinga. Kulingana na uamuzi wa majaji, hili ni jambo ambalo lilienda kinyume cha sheria kulingana na kifungo cha 257 katika katiba ya Kenya. Kamati iliyoundwa kusimamia mchakato wote iliundwa kinyume cha sheria na ilikuwa kamati haramu tangu mwanzo. Pia walishutumu hoja kwamba, rais mstaafu Mwai Kibaki alianzisha mabadiliko ya kikatiba mwaka 2005 na 2010. Majaji hao walisema kwamba, rais Kibaki alifanya hivyo kupitia katiba ya zamani. Katika katiba ya sasa, walisema kwamba, inasema ni nani anayeweza kuanzisha mpango wa kubadili katiba, walisema. ***''Katiba inasema ni nani anayeweza kufanya mabadiliko. Rais ama chombo cha serikali sio kati ya wanaopatiwa fursa hiyo''***. Wakuzaji wa BBI waliambia mahakama kwamba rais alikuwa akitumia uwezo wake kikatiba alipoanzisha mchakato wa BBI. Lakini mahakama ilisema kwamba, bwana Kenyatta alifeli kulinda katiba na hivyo basi, akakiuka katiba katika masuala ya uongozi na maadili. Huku juhudi zake za kuunganisha taifa zikipongezwa, katika majukumu yake hawezi kuanzisha mpango wowote wa kufanyia marekebisho katiba kinyume na katiba. Hana uwezo kama huo. Waliongezea kwamba mchakato huo tangu mwanzo haukufuata sheria. Mahakama hiyo pia ilisema kwamba, rais aliyepo madarakani anaweza kushtakiwa binafsi iwapo ataenda kinyume na sheria, kwa vitendo vyake.

Je, umma ulishirikishwa? Majaji walisema kwamba rais Kenyatta aliorodheshwa kama mtuhumiwa na alishirikishwa katika kesi hiyo hadi mwisho. Hivyo basi, kuhusu mahakama hiyo iliamuru kwamba shughuli yote ilikwenda kinyume na sheria kwa sababu wakuzaji wa BBI walishindwa kuwashirikisha Wakenya. Kulingana na maoni ya Kenyatta, kuleta utulivu na amani nchini kenya ilikuwa jambo la maana sana ambalo, lingefanya akumbukwe hata baada ya kustaafu. Mwanafunzi mmoja alipomuuliza Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta mwaka wa 2018 kuhusu jinsi ambavyo angependa kukumbukwa atakapoondoka madarakani, alionekana kupatwa ghafla na swali hilo, kabla ya kutaja mambo mawili. "***Moja ni kwamba nitakuwa nimeacha jamii iliyoungana, yenye mshikamano. Na pili, kwamba tutakuwa tumeshinda vita dhidi ya ufisadi".*** Hatua muhimu zaidi kuelekea umoja wa kitaifa ilikuwa Machi 2018 alipopeana mkono na kiongozi wa upinzani na aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga, kama ishara ya mapatano yao ya kisiasa. Kusalimiana ***"Handshake"*** kulimaliza miezi kadhaa ya sintofahamu na machafuko kufuatia uchaguzi ambao ulibatilishwa na Mahakama ya Juu 2017, na uchaguzi wa marudio ulisusiwa na Bw Odinga, ambaye aliendesha sherehe zake ya kuapishwa ya katika mji mkuu a Nairobi.



*Raila kuapishwa*

Mapatano ya Kenyatta na Odinga hayakupokelewa vyema na Naibu Rais William Ruto, ambaye alidai kwamba yalivuruga ajenda yao madhubuti ya kuimarisha usalama, kuongeza chakula, kufikia huduma ya afya kwa wote, kujenga nyumba za gharama nafuu zaidi, na kukuza sekta ya viwanda. Jambo hili hatimaye lilisababisha wawili hao kutofautiana, huku Bw Kenyatta akiondoa uungaji mkono wake kwa Bw Ruto na badala yake kumuunga mkono mpinzani wake Bw Odinga, kuwania urais katika uchaguzi wa 2022. Mvutano kati ya Bwana Kenyatta na naibu wake uliendelea hata baada ya uchaguzi. Kenyatta alikataa kutoa pongezi hadharani kwa Bw Ruto kwa ushindi wake, ingawa alisema atafanikisha mabadiliko ya mamlaka kwa njia ya amani.

Huenda umoja ambao Bw Kenyatta alitafuta haukutokea jinsi ambavyo angetaka, lakini wachanganuzi wa mambo ya siasa walisema, ulikuwa muhimu kwa nchi ambayo imejaribu kujiepusha na ghasia zilizoenea kati ya makabila ambayo yalizuka kufuatia uchaguzi wa 2007 uliozozaniwa, ambapo takriban watu 1,200 walikufa na maelfu ya wengine walilazimika kuyakimbia makazi yao. Huku uchaguzi uliokuwa umekamilika hivi punde kufanyika kwa amani, wadadisi waliamini kuwa Bw Kenyatta alifanikisha azma yake ya kuleta umoja na kujenga jamii yenye mshikamano, licha ya mgombea wake Bw Odinga kushindwa katika kinyang`anyiro cha urais

Kusalimiana kwa mikono kulizua hisia ya ushirikishwaji, kwa sababu kama kungekuwa na kitu chochote ambacho kingeigawanya nchi hii na kuitupa katika kaburi la sahau, ilikuwa wazo zima la baadhi ya watu kuhisi kutengwa - wazo kwamba serikali ni ya sehemu fulani ya watu au jamii. Makubaliano haya, hata hivyo, yaliacha pengo katika upinzani, kwa sababu yaliongeza mgawanyiko juu ya nani alikuwa serikalini na nani hakuwepo. Ukosefu wa upinzani mkali wa kuangalia ubadhirifu wa serikali huenda ulichangia katika kushindwa kwa Bw Kenyatta, kukomesha ufisadi na ufujaji wa

rasilimali za umma. Alipokuwa akimpigia debe Bw Odinga, alikiri kwamba, amekuwa mpole katika kushughulika na wafisadi. Mnamo 2021, alisema nchi ilikuwa ikipoteza takriban shilingi bilioni 2 za Kenya ($17m; £14m) kila siku kutokana na ufisadi.

Utawala wa Bw Kenyatta uliwekeza pakubwa, katika misingi kote nchini na miradi inayoanzia mabwawa makubwa, viwanja vya michezo, viunganishi vya umeme, reli na barabara kama vile Barabara ya Nairobi Expressway. Uwekezaji huu uliwezekana kwa kukopa kwa wingi, lakini maswali yaliibuka kuhusu gharama zilizotumika, thamani ya fedha na mapato ya uwekezaji kwa wananchi.

Kwa mfano, Reli ya Kisasa ya Standard Gauge (SGR) iliyojengwa na wachina kutoka mji wa pwani ya Mombasa hadi Nairobi iligharimu mlipa ushuru $3.2bn (£2.8bn), ambayo wachambuzi wanahoji kuwa, ilikuwa ya bei kubwa ikilinganishwa na miradi kama hiyo, iliyotekelezwa na majirani wa Kenya, Tanzania na Ethiopia. Ukopaji huo ulisukuma deni nchini hadi kufikia viwango vya juu, ambapo nchi italazimika kulipa kwa miaka ijayo. Mwishoni mwa 2021, deni la nchi lilifikia $72.6bn, sawa na 68% ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na 38% ya Pato la Taifa wakati Bw Kenyatta alipochaguliwa kuwa rais 2013. Lakini watalamu wa mambo ya fedha waliashiria ya kwamba, hakuna ubaya kuwa na deni, suala ni jinsi gani hizo pesa zinavyotumika.

Ingawa kulikuwa na ukosoaji wa mabadiliko hayo, mfumo huo mpya ulinuiwa kuibua uwezo wa ubunifu wa wanafunzi kwa kuwapa ujuzi watakaohitaji kupata kazi, badala ya kuzingatia kufaulu kwenye mitihani tu. Na wakati mpango kabambe wa kusambaza huduma za afya kwa wote nchini haujatekelezwa kikamilifu, uwezo wa vitanda vya hospitali kumeboreshwa kwa kiasi kikubwa na hospitali mpya kujengwa. Mbali na mandhari ya ndani, kimataifa, hadhi ya Kenya iliimarika katika muongo uliopita.

Huku Bw Kenyatta akikabidhi hatamu za uongozi kwa Raisi mteule William Ruto, changamoto kwa serikali ya Ruto ilikuwa sio tu, kutekeleza baadhi ya ahadi kubwa walizotoa, kwa wapiga kura wakati wa kampeni, bali pia kushughulikia baadhi ya mahitaji muhimu yanayowakabili wananchi. Hizi ni pamoja na ukosefu mkubwa wa ajira na kupanda kwa gharama ya maisha, huku mfumuko wa bei ukipanda hadi rekodi ya juu ya 8.5% mwezi Agosti mwaka wa 2023



*Rais wa tano wa Kenya – William Ruto*

Wakosoaji wa Bw Kenyatta walisema kuwa, wakati wa uongozi wake aliwazuia kuwa na uhuru wa kujieleza na ule wa wanahabari. Mwaka 2016, mwanahabari wa gazeti la kibinafsi linalosomwa zaidi Kenya, Daily Nation, alifutwa kazi kwa kuandika tahariri ambayo ilikosoa serikali. Godfrey Mwapembwa, mchoraji vibonzo, maarufu kwa jina Gado, naye alidaiwa kufutwa kwa kuchora vibonzo vilivyoikosoa serikali mara kwa mara. Kiuchumi, swali kuu ni: Wakenya wako heri sasa kuliko walivyokuwa mwaka 2013? Uchumi wa Kenya ulikuwa ukikua kwa kiwango cha wastani cha asilimia 5 kila mwaka tangu aingie uongozini, lakini baadhi ya Wakenya walisema hawajahisi manufaa ya ukuaji huo.

Unga wa mahindi uliadimika na kupanda bei, hadi ukailazimu serikali iingilie kati. Kwa miezi mitatu hivi, kulikuwa na uhaba mkubwa wa unga wa mahindi na gharama ya bidhaa nyingi muhimu zilipanda. Serikali yake pia ilituhumiwa kuchukua mikopo kwa wingi, baadhi wakikadiria kwamba, serikali hiyo ilipitisha viwango vya ukopaji vya serikali zote za awali tangu uhuru. Deni la wakati wa utawala wa Kenyatta lilifikia $26bn (£20bn). Bw Kenyatta, hata hivyo alisema kuwa uwekezaji wa pesa hizo katika miradi ya miundombinu, mfano reli ya kisasa kutoka Mombasa hadi Nairobi iliyogharimu $3.2bn (£2.5bn), ingesisimua ukuaji wa uchumi. Rais Kenyatta aliahidi kuangamiza ufisadi lakini, mwanaharakati John Githongo alisema kuwa, serikali ya Kenyatta ilikuwa ndiyo "fisadi zaidi katika historia ya Kenya". Katika ripoti ya maoni kuhusu viwango vya ufisadi ya 2016 Transparency International Kenya iliorodheshwa nambari 145 kati ya nchi 176. Bw Kenyatta alikuwa akisema kuwa juhudi zake za kukabiliana na ufisadi zimehujumiwa na mahakama na mamlaka ya kupambana na rushwa.

Mwaka 2015, Kenyatta aliwasimamisha kazi na kisha akawafuta mawaziri watano na maafisa wengine wa ngazi ya juu ya serikali, waliotuhumiwa kujihusisha katika ufisadi. Waziri mwingine alijiuzulu kutoka na shinikizo kutoka kwa umma.

Bwana Uhuru alifanikisha utawala wake kwa njia iliofaa kama kiongozi wa nchi na jenerali mkuu wa jeshi. Makosa aliyoyafanya bwana Uhuru ni kuonyesha kujipenda, badala ya kuonyesha ama kukubali kuwa ameshindwa, na kuelimisha watu wamkumbatie aliyeshinda na kumbariki, na kukumbali demokrasia ya nchi. Bwana Uhuru aliukabidhi uongozi kwa shingo upande, jambo ambalo lilisababisha kuwepo kwa mwanya, kwa upinzani kuleta vurugu kwa muda. Bila kuwa na uwoga wa kuonywa na umoja wa mataifa kwani, hakuna hatua madhubuti wangewachukulia kwa kufanya haya yote.

## **Umoja wa Mataifa**

Tokeo moja lilopewa umuhimu kutokana na vita vya pili vya dunia, lilikuwa la kuanzishwa kwa muungano wa Umoja wa Mataifa. Huu mungano uliundwa katika mwaka wa 1945 ukinuwia kuwa chombo muhimu cha kuzuia vita kwa wakati ujao. Kutokana na historia hii, mataifa yaliyokuwa na nafasi za kudumu na kura ya VETO katika Baraza la Usalama ndiyo yaliokuwa ni mataifa washindi wa vita vikuu vya pili: Ufaransa, Marekani, Ufalme wa Muungano na Urusi na vile vile uchina. Katika muungano huo wa Umoja wa mataifa ndio ulinuiwa kuzima vita vya wenyewe kwa wenyewe, na taifa kwa taifa. Umoja huu, ulikusudiwa kudumisha haki na heshima kwa binadamu. Kwa hivyo, muungano huu, unafaa kua na nguvu ya kushtaki wenye kuleta vurugu kwa nchi tajika.

## **Jitihada za Jumuiya ya Kimataifa**



*Picha ya kongamano la umoja wa mataifa*

Katika mwaka wa 2017, Katibu Mkuu wa Umoja wa mataifa António Guterres alitoa maoni yake yaliyolenga ripoti kutoka kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Katika ripoti hiyo, ilidhihirika wazi kuwa kikundi cha kigaidi kilichoko nchini Somalia

kinachojulikana kama Al-Shabaab kilitegemea wanajeshi watoto kwa njia kubwa katika uvamizi wake. Katika ripoti hiyo, pia ni dhahiri shahiri kwamba, zaidi ya asilimia 50 ya nguvu ya mapigano katika wanamgambo wa Al-Shabaab ilijumuisha wanajeshi ambao ni watoto. Vile vile katika ripoti hiyo, iliibuka kuwa, katika kikudi cha kigaidi cha Al-Shabaab, kuna watoto wengi zaidi wa umri wa chini ya miaka tisa. Watoto wanawekwa katika mstari wa mbele katika vita na vile vile migogoro mingi.

Ripoti hiyo ilikuwa na umuhimu zaidi kwani ilithibitisha kwamba, ni takriban watoto 6,163 ambao waliajiriwa na kutumiwa katika mapigano pamoja na migogoro mingi kati ya tarehe 1, mwezi wa Aprili, mwaka wa 2010 na mwezi wa Julai, tarehe 31, mwaka wa 2016. Kati ya watoto hao, ilikadiriwa ya kwamba, idadi ya 230 walikuwa ni wasichana. Vile vile ni dhahiri kwamba, kikundi cha Al-Shabaab waliajiri watoto 4,213. Kati ya watoto hao wote, ilikadiriwa kuwa asilimia sabini ya kesi hizo zimethibitishwa. Fauka ya hayo, Jeshi la Kitaifa la Somalia waliajiri watoto takriban 920.

Kabla ya ripoti hiyo, katika mwaka wa 2010, shirika lisilo la serikali kubwa la waangalizi wa haki za kibinadamu ambalo linajulikana kama mtazamo wa haki za binadamu ("**Human Rights Watch**") kwa Kingereza liliripoti kwamba, kikundi cha kigaidi cha Al-Shabaab, kilikuwa kina waajiri watoto wenye umri wa miaka kumi, ili kushiriki katika vita na migogoro yao. Watoto hao walikuwa, wakitekwa nyara kutoka manyumbani na shuleni mwao, Mara nyingi darasa nzima la watoto lingetumiwa kama wanajeshi katika vita na vurugu.

Katika mwaka wa 2012, kiongozi msaidizi wa shirika lisilo la serikali kubwa linalojulikana kama watetezi wa kimataifa ama "**Amnesty International**" aliyejulikana kama Michelle Kagari alisema kwamba, "Somalia sio tu mgogoro wa binadamu hata, pia ukiukaji wa haki za kibinadamu na haki za watoto. Watoto wa Somalia hukabiliwa na hatari ya kifo kila wakati: kwa mfano, inawezekana kwamba watoto hao, kuajiriwa na kupelekwa kwenye mstari wa mbele vitani. Inawezekana kwamba wao waliadhibiwa na Al-Shabaab, kwa sababu wanasikiza muziki, au 'kuvaalia nguo mbaya'. Mara nyingi wao wanalazimishwa kujitunza peke yao, kwa sababu ya kufariki kwa wazazi wao. Watoto wengi hupoteza uhai wao kwa sababu hawapati huduma na matibabu ya kutosha." Vita au vurugu yaweza kumalizwa na ulimwengu kwa kuweka masharti kwenye nchi tajika iwapo ipo mwanachama.

Uhai na ufanishi katika maisha ya mwanadamu hua na umuhimu mkubwa. Kwa hivyo, ni vizuri nchi yote iwe kwa muungano wa mataifa, kuhimiza viongozi wa utawala, kufuata na kutimiza yanaoabatana na ubora wa maisha.

# SURA YA 15: UBORA WA MAISHA KWA ULIMWENGU



*Watu wenye majukumu tofauti*

Ili maisha yawe bora na ya kuridhisha raia, kanisa, watumishi wa umma na wanasiasa wanafaa kujumuika pamoja ili watu wasaidike na umoja wao. Hii ndio, waweze kuelimisha raia wakiwa pamoja. Huu muungano ukiwa pamoja itapata nguvu ya kuelimisha na kushauri mambo haya: -

- Watu wako na haki ya kuishi na kukakaa mahali popote nchini.
- Kuuliza na kujua hali ya maisha ya binadamu.
- Wako na haki ya kushikilia na kuhifadhi mali wakiwa mahali popote.
- Wako na haki ya kukuza raslimali yao bila kutishwa.
- Watu wako na haki kujua kwamba hakuna umbaguzi wa sura ama kabila.
- Kila mmoja ana haki ya kulindwa na kupata matibabu.
- Kila mtu ako na haki ya kukutana na wale wengine na kujieleza.
- Kila mtu ako na haki ya kwenda mahali popote nchini bila kuzuiliwa.
- Kila mtu ana haki ya kufanya kazi ama biashara popote nchini
- Kila mtu anaweza kuendeleza ama kukuza mahali popote yuko.

- ❖ Kila mtu ako na haki ya kuwa na familia katika mahali popote nchini
- ❖ Kila mtu ako na haki kupata huduma njema kutoka kwa watumishi umma.
- ❖ Kila mtu kama amefungwa lazima apate haki ya kukula na kupata matibabu.
- ❖ Kila mmoja ako na haki ya kukosoa, kuuliza na kushauri serikali kwa maendeleo ya nchi.

Haya yote ndio yanafaa kuzingatiwa na viongozi wote, wa nchi na himizo hii iwe kwa viongozi tawala, ndio maisha ya raia iwe bora. Vilevile ni vizuri viongozi wa UN (Umoja wa mataifa) kua na wazo hili kwa ulimwengu, ndio iwe himizo kwa nchi mwanachana.

- Ulimwengu kuhimiza nchi kutunza mtoto yeyote aliyezaliwa katika nchi tajika na wazazi wa nchi nyingine bila kumbagua kwa misingi ya rangi, kabila wala dini iwapo mzazi wake ashafariki. Viongozi wa nchi kuwa waangalifu, ili wasiharibu vivutio vya utalii na uchafuzi wa mazingira.
- Ulimwengu kuhimiza nchi kuhusu haki za raia, kwa watumishi wa umma, kwa kupewa haki, amani na ushauri mwema.
- Ni vizuri ulimwengu kuhimiza nchi tajika kuwa na mpangilio mzuri wa nyumba ili kuepusha uchafuzi wa mazingira. Hii itasaidia raia kukaa katika mazingira bora na safi.



*Nyumba Za Bei Nafuu Kwa Wananchi*

- Ulimwengu kuangalia uongozi wa nchi ili usiumize raiya wake, kwa makosa ya uongozi wa hapo awali, mbali wagharamie na kushtaki mwenye makosa.
- Kwa kudumisha haki na heshima ya binadamu, serikali ya inchi tajika yafaa, kuweka mipaka au alama kwa raslimali yake na ya umma, ili kuwazuia raia kundanganyika na baadaye kubomolewa makaazi yao na kisha kupata hasara .

- Viongozi wa ulimwengu wanafaa, kuhimiza nchi tajika kuwapa raia wake vyeti vya ugavi na umiliki, ili kuondoa migogoro baina ya raia. Kwa haki na utaratibu wa nchi, viongozi wa nchi hawafai kutumia idara zozote za serikali katika siasa au kutisha raia wake, ili yale wananchi hawataki yaendelee.
- Ulimwengu kuhimiza viongozi wa nchi, kutunza na kuhifadhi desturi ya heshima. Vile vile, sheria iwatambue viongozi wafisadi, ili ukweli usichanganyike na siasa. Hivyo basi, raia watafahamu, kwa kina ukweli na uongo.
- Ulimwengu kuhimiza mke na mume, kuwalea watoto kwa pamoja, ili wanao wawe wakamilifu katika maisha. Pia kufunza nchi, utawala wa sheria katika kuwatumikia raia, nao wautii na kuufuata, ili kuboresha maisha.
- Ulimwengu kuhimiza elimu bora na mazingira bora kwa mtoto, kama haki yake ya kimusingi wa maisha.
- Ulimwengu kuimarisha usawa katika huduma za uma na kupigana na ufisadi. Hivyo basi, kuhakikisha ugawaji wa rasilimali katika maeneo mbalimbali, umefuata kanuni za mipaka na kudumisha haki kwa wote.

- Ulimwengu kuhimiza nchi zizingatie mambo ya mipaka ili migogoro ya aina hiyo isijitokeze. Kwa mfano, mgogoro wa mipaka kati ya nchi ya Kenya na nchi ya Somalia na zinginezo ulimwenguni.
- Viongozi wa ulimwengu wafaa, kuhimiza heshima kwa viongozi tawala wa nchi na kuelimisha dhidi ya manufaa yake kwa raia, ili kuipa nchi utulivu na nafasi ya maendeleo.
- Heshima ni msingi wa maisha kwa binadamu, uhai na vyote anavyohitaji. Jambo hili limehamasishwa kwa sababu ulimwengu umeanza kupotoka na kujihusisha na ulanguzi wa binadamu kiholela. Ili kuhifadhi ubora wa maisha mema kwa binadamu, ulimwengu uzuilie nchi kukuza na kuuza dawa za kulevya kwani, mazao yake huwa shida, kwa dunia na nchi kijumla.
- Dunia na viongozi wake wamejaribu kufanya kongamano zinazoghusia mambo haya yote lakini shida imetokana na kutotekeleza ili kuboresha maisha ya raia. Kwa mafano, kongamano la Madhara ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa mkutano wa COP, uliojadilia maswala ya changamoto kubwa za mabadiliko ya hali ya hewa.

Upandaji wa miti na kuzuia umonyonyoko wa udongo ni msingi bora wa maendeleo, kwa kupata hewa nzuri na manufaa mengi kwa binadamu na pia wanyama. Miti husaidia kuzuia upepo na jua kali.

- Kusambaza maji - Maji ni kiungo muhimu katika maisha ya binadamu na wanyama, kwa hivyo serikali inafaa kutafuta binu mwafaka ya kupata maji ya kunywa na ukulima, ndio watu wapate chakula na usafi.



*Huduma ya maji kwa wananchi*

- Dini ni kiungo muhimu katika maisha ya kila mmoja. Hivyo basi, ulimwengu wafaa kudumisha uhusiano mwema na heshima kati ya serikali na dini ili pamoja ziweze kuangazia yanayohusu binadamu. Basi, jambo la muhimu litakuwa kuangazia mambo yanayonyima jamii heshima, haki, afya na amani. Ulimwengu kusisitiza kuwa, utalawa wa sheria unapaswa kuleta matokeo yanayotarajiwa na ya kufaa katika utendaji wa serikali.
- Ili ulimwengu kuweza kumaliza ugaidi, ni lazima nchi zote zishikane mikono na kuvamia vikundi vya ugaidi kabla havijapata nguvu zaidi na kuvamia nchi mbalimbali. Vile vile, umoja wa mataifa waweza kuwachukulia hatua na kuwaadhibu wafadhili wa vikundi hivyo haramu, baada ya kuchunguza chanzo chao.
- Kwa ubora wa maisha na heshima kwa binadamu na uhuru wao, maandamano yanayofanyika katika nchi, lazima yaidhinishwe na mashirika ya nchi husika, angalau robo tatu, hasa mashirika ya kidini, shirika la kutetea haki za binadamu na mengineyo kulingana na himizo la ulimwengu.
- Inafaa viongozi wa ulimwengu kuhimiza heshima kwa misingi ya desturi na utamaduni, kwa nchi tajika, ili uzao uweze kuiga kama kinga yao kwa jamii.



*Baraza la wazee*

- Heshima kama kiungo muhimu katika raia, serikali inafaa kuonyesha na kutambua kwa heshima wazee, kuwatunza na kuwashikanisha na kizazi chao badala ya kuwatenganisha.

- Ulimwengu kuhimiza nchi kushughurika na mienedo ya madhehebu, kabla ya majanga kutokea, na wala sio baada ya vifo vya halaiki ya watu, kutokana na wahubiri wapotovu.
- Ulimwengu kuzipa nchi ushauri wa dhamana na busara, ili zitambue jinsi ya kuimarisha haki inayozingatia maisha bora.
- Viongozi wa ulimwengu kufuatilia uchaguzi wa nchi ili kuziepusha na vita vya baada ya uchaguzi na vile vile kuepusha watumishi wa uma kuwachochea raia.
- Jambo la dawa za kulevya kujadiliwa na ulimwengu kwani limeadhiri maisha ya vijana wengi na kuwafanya watumwa na wahalifu.
- Ni vizuri kuwachunguza wanaotengeneza makombora, ili kulinda haki na uhai wa binadamu na kuwafanya watengenezaji hawa, wasipotoke na kuangamiza ulimwengu.
- Ulimwengu kukubali kujihusisha katika michezo baina ya nchi tofauti kama mtindo kuleta pamoja watu kwa urafiki bila ubaguzi.
- Viongozi wa ulimwengu kufuatilia miundomsingi ya barabara, ndio kusaidia mawasiliano na mwangaza katika jamii, ili watu wapate maendeleo na wajuane.



*Ubora wa barabara*

- Ni vizuri ulimwengu kuwa na wataalamu wa pamoja kama vile wa anga, ili kilimo-biashara, isaidie ulimwengu wote. Jambo hili, litachangia pakubwa katika kuwezesha nchi kuepuka janga la njaa, kila nchi kujimudu kibiashara na mambo mengine ya maisha. Ulimwengu kutilia maanani, kwa mambo ambayo huchangia pakubwa katika kuharibu ubora wa maisha. Mambo hayo ni kama ulanguzi wa binadamu, jambo ambalo huwapata wasiojua. Watu hao hujipata, katika mtego wa ulanguzi huo na kupoteza maisha yao. Basi, ni vyema kwa watu kushauriwa vilivyo, ili kuepukana na mitego hiyo

- Ulimwengu kuangalia matendo mengine yanayojitokeza wakati wa vita, kama vile kuwatelekeza raia, na askari kuwabaka kina mama na watoto. Hivyo basi, ulimwengu ulinde haki na uhai wa binadamu, kwa kutafuta mbinu ya kuzuia migogoro kwa amani kwani, maisha na mali yao ni ya dhamana kubwa. Jamii imara hupatikana iwapo haki za binadamu zitahifadhiwa na majukumu kutekelezwa. Pia, uchafuzi wa mazingira unapaswa kuangaziwa kwa upana, ili hali ya anga isije ikabadilika.

Shirika la chakula na kilimo ulimwenguni (Food and Agriculture Organization - FAO) linaeleza kuwa, ili kujitosheleza kwa hali ambayo watu wote watapata vyakula, ni lazima watu wapate usalama na masomo ya kilimo-biashara. Mwakani 2022 kamati ya Oxford kuhusu janga la njaa (Oxford Committee for Famine Relief - OXFAM) walikariri kuwa, watu milioni ishirini na moja wamekumbwa na njaa pamoja na mifugo yao kwa sababu ya ukame na ugonjwa hatari wa Covid-19. Waliendelea kusema kuwa juhudi za kujitosheleza kwa chakula zinategemea kutekelezwa kwa sera zilizopo za kumaliza majanga, kama mafuriko, ukame na ufisadi.

Hali hii imechangia pakubwa kwa wakulima kulinda mimea yao ili isinyauke wala kukaukia mashambani. Basi, kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika kuwawezesha watu kutosheleza chakula, viongozi wa nchi kadhaa za bala la Afrika walipatana Maputo, Msumbiji mnamo 2003 na kutoa mkataba sahihi. Ili Afrika kujitosheleza kwa chakula, mkataba huo ulitaka kila taifa lililokuwa mwanachama wa muungano wa Afrika liahidi kutenga kilimo na kuhakikisha ustawi wa maeneo ya mashamba angalao kwa asilimia kumi (10%). Haya yote ni mawazo mazuri ya kumsaidia mwanadamu, lakini inafaa ulimwengu ushirikiane, ili wanadamu katika pembe zote za dunia wasaidike.

Ili ulimwengu ukue katika maendeleo ya aina zote za kimaisha, kila taifa lahitajika kufanya maendeleo, kwa kujitolea na kuajibika kikamilifu kwa moyo wa kuwajali wenzao, lazima wawe na wataalamu ndio nguzo kubwa ya maendeleo ya nchi tajika, kwani wao hupeana mwelekeo wa maendeleo. Wao pia huchangia kwa kupanua mawazo ya watu kwani, kuna mambo mengi yanayokwaza maendeleo na kuharibu uchumi wa nchi.

Basi, nchi zapaswa kuwapa wataalamu vifaa vya kazi vya hali ya juu, kulingana na kazi ya kila mmoja. Wajibu wa raia unahusu matendo na mchango katika utawala wa kidemokrasia na ushirika katika shughuli za maendeleo za nchi tajika. Basi, raia wanapaswa kuendeleza ukarimu, uaminifu na moyo wa uzalendo, bila kupuuza mawazo ya wataalamu wa; hali ya anga, elimu, kilimo, dini na hata afya.

**1. Hali ya anga**



Wataalamu hutayarisha mipangilio itakayowaongoza watu ama nchi kwa kueleza watakavyopokea misimu tofauti. Hili huchangia pakubwa kwa kuwasaidia watu ama nchi kuepukana na majanga ya njaa. Wakati mwingine, wataalamu wanaweza kudanganyika, kama hawana vifaa ama wakati wa kutosha wa kufanya uchunguzi. Hivyo basi, baa la njaa laweza kuikumba nchi husika.

**2. Elimu**



*Mafunzo kwa wanafunzi*

Elimu ni jambo lenye umuhimu sana kwa mwanadamu. Hivyo basi, elimu hutegemewa kwa kuerevusha watu. Vile vile, elimu hupeana maono na mawazo mazuri yanayonufaisha maisha ya binadamu.

**3. Kilimo**



*Ukulima kwa njia ya tecknologia*

Kilimo ndicho kitega uchumi kwa mataifa mengi duniani. Katika nchi zenye mikataba ya kilimo na nchi zingine na pia katika nchi zinazotegemea kilimo peke yake. Kuna wataalamu wengine ambao hushughulikia mipaka. Ulimwengu unapaswa kuwapa nafasi ya kuepusha nchi kupata hasara kwa sababu ya vita vinavyozuka kwa ajili ya mipaka inayotumika katika ukulima. Hili husaidia kukuza urafiki na heshima kati ya mataifa tofauti na kuleta maendeleo ya kilimo baina yao.

**4. Dini**

Dini huwafanya watu tofauti kuheshimiana na kuishi pamoja, kwa amani kama ndugu katika ulimwengu. Hivyo basi, wataalamu wa dini hutegemewa kusomesha, kuelekeza na kuleta amani, ili watu waweze kuimarika katika maisha yao ya kiroho na kimwili. Dini hufunza wanadamu kutotofautisha rangi, kabila na mambo mengine ambayo huchangia pakubwa katika kutenganisha watu. Vile vile, dini huifanya dunia iwe ya kufaana, kwa sababu watu huwa na uhuru wa kuishi na kuabudu pamoja. Dini pia huwaelimisha watu kufanya maamuzi yenye ukweli na yanayozingatia utu na isitoshe huwapa wanadamu moyo wa kuishi na matumaini.

**5. Afya**



*Hospitali*

Ulimwengu hutegemea afya kama nguzo muhimu katika maisha, kwani uzuri wa maisha hutegemea ubora wa afya. Basi, nchi zinazowadhamini raia wake hujaribu mbinu zote zinazoweza kudumisha afya ya umma. Ili watu wakue na kuishi kwa afya njema, nchi tajika huhakikisha imepiga marufuku dawa za kulevya na vitu vyovyote vyenye uwezo wa kuadhiri afya na maisha ya binadamu. Hatimaye nchi kama hiyo hupigana na ufisadi unaoambatana na kuibiwa kwa dawa hospitalini na mambo mengine kama hayo, ili wananchi wote wafaidike kwa matibabu ya hali ya juu

Hospitali ndio hudumisha afya ya binadamu ikiwa na matibabu bora. Kwa hivyo ni vizuri nchi yoyote kuhakikisha haki ya binadamu ili kutimiza wajibu wake.

## SHUKRANI

Ninatumia nafasi hii ili kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kwa njia moja au nyingine kuandika kitabu hiki. Kwanza kabisa, ningependa kumpa kongole Mwalimu Kennedy Isoe Onyinkwa kwa kazi nzuri na kujitolea mhanga ili kutafsiri na kukikariri kitabu hiki, na vile vile Jorum Macharia, Kennedy Macharia, Joseph Kimemia, na wakiwa ni pamoja na Anthony Kuria kwa kukipiga chapa.

Ningependa kushukuru kamati ya utendakazi wafuatao kwa mchango wao wa dhati;

Bwana Peter Kamau – Mwalimu

Bwana Julius Kimani – Mwanabiashara

Bwana Alex Karanja – Mwalimu

Bwana Festus Maina – Mkulima

Bwana Francis Njoroge Macharia – Mfanyikazi wa umma

Bi Sarah Wangechi Ng‟ang‟a – Mkulima

Haya ni mambo ambayo yamejaribiwa kufafanuliwa katika maisha ya mwanadamu. Ingawa kuna mengine, hayajanakiliwa na mwandishi wa nakala hii.